# Nipashe

Jumatatu Desemba 9, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580096

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



Albinism Hotline

• Jifunze kuhusu Ualbino

• Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

CEFA

215544702




## Ali Mufuruki afariki dunia, vigogo wamlilia kila kona

UKURASA 3

# DC aagiza kushushwa bendera zote upinzani

• **Aamuru** zibaki za CCM, vyama vyamjia juu, Msajili asema... *Endelea ukurasa 2*


Uongozi na wafanyakazi wa gazeti hili tunawapongeza wasomaji, watangazaji na Watanzania wote kwa kuadhimisha miaka 58 ya Uhuru.


## Serikali kushusha gharama za umeme

UKURASA 3



Rais John Magufuli, akimsikiliza msimamizi wa mradi wa ujenzi wa chelezo na ukarabati wa meli za MV Victoria na Butiama katika Ziwa Victoria, Meja Abel Gwanafyo, alipokuwa akitoa maelezo kuhusu miradi hiyo kwenye sherehe za uwekaji mawe ya msingi katika eneo la Bandari ya mizigo Igogo, jijini Mwanza jana. **PICHA: IKULU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## JPM: Mafisadi bado wapo, tutaendelea kuwakamata

UKURASA 2


**MICHEZO** MO ACHARUKA ATANGAZA TIMUATIMUA UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Chadema yapitisha wagombea mabaraza

**Na Enock Charles**

KAMATI Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), imewapitisha vijana watatu kati ya tisa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Baraza la Vijana la chama hicho (Bavicha), huku kigezo cha kutokujua lugha ya Kiingereza na umri vikitumika kuengua wagombea sita.

Mkurugenzi wa Mambo ya Nje, Itikadi na Uenezi wa Chama hicho, John Mrema, alisema mgombea katika nafasi ya uenyekiti wa baraza hilo ni muhimu afahamu lugha za kigeni hasa Kiingereza ili kukiepusha chama usumbufu wa kumtafutia mkalimani anapotakiwa kwenda katika mikutano nje ya nchi.

"Tunatarajia mwenyekiti wa baraza la vijana awe ni mtu ambaye tunaweza tukamtuma kwenye mkutano wowote wa kimataifa bila kumtafutia mkalimani kwa hiyo Kamati Kuu ilizingatia hilo kama mojawapo ya vigezo."

INAENDELEA UK. 7



Askofu wa Kanisa la Mlima wa Moto, Mikocheni B, Assemblies of God, Dk. Getrude Lwakatare, akifungua kongamano la siku saba la kuliombea taifa amani akiwa na baadhi ya wachungaji wa kanisa hilo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# DC aamuru bendera za upinzani kushushwa

**Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Sumbawanga mkoani Rukwa, Dk. Halfan Haule, amewaagiza wenyeviti wa serikali za mitaa na vitongoji Manispaa ya Sumbawanga kuondoa bendera zote za vyama vya upinzani na kuziacha za Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kuwa ndiyo chama tawala.

Kutokana na agizo hilo, vyama vya upinzani nchini vimemjia juu kiongozi huyo na kumtaka kutambua kuwa vipo kisheria na vina haki ya kupeperusha bendera zao, huku vikisubiri kauli ya Msajili wa Vyama vya Siasa, ambaye alisema hadi sasa hana taarifa rasmi na hawezi kulizungumzia.

Agizo hilo alilitoa mwishoni mwa wiki, baada ya wenyeviti hao kula kiapo katika ukumbi wa mikutano wa manispaa hiyo.

Akihutubia wenyeviti hao, aliwaagiza kuzing'oa bendera zote za vyama pinzani kwa madai kuwa zitakuwa zikiwachanganya wananchi, watashindwa kufahamu ni wapi viongozi hao wanapatikana.

Alisema kwa kuwa CCM ndiyo chama kilichoshinda uchaguzi kwa asilimia 100, hakuna sababu ya bendera za vyama vingine kupeperushwa, huku akiahidi kupita mitaani kukagua utekelezaji wa agizo lake.

Kwa mujibu wa Dk. Haule, utekelezaji wa agizo hilo ni mkakati wa kuhakikisha hata katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 hakuna diwani atakayeshinda kutoka chama cha upinzani.

INAENDELEA UK. 8


## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO LA UUZAJI WA VIWANJA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote kuwa zoezi la upimaji wa viwanja limekamilika na kuanzia **TAREHE 3/12/2019** viwanja vitaanza kuuzwa kila siku za Jumatatu hadi Ijumaa katika eneo la wazi la Manispaa ya zamani (karibu na Sabasaba) kuanzia saa 2 Asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri.

**Viwanja vinavyouzwa ni katika maeneo ya:**

| ENEO | MATUMIZI NA BEI TSHS KWA (SQM1) |
|---|---|
| NALA (Karibu na Chuo cha IFM na Kituo cha kupaki Malori) | • Makazi 4,000/= <br> • Makazi na Biashara 5,000/= |
| CHAHWA (Karibu na Ikulu) | • Makazi 3,000/= <br> • Makazi na Biashara 5,000/= |
| Mahoma Makulu (Nyuma ya Mji wa Serikali) | • Makazi 3,000/= <br> • Makazi na Biashara 5,000/= |
| KIKOMBO (Karibu na Bandari kavu na Makao Makuu ya Ulinzi ya Taifa) | • Makazi 2,000/= <br> • Makazi na Biashara 3,500/= |
| MTUMBA (Karibu na Mji wa Serikali na Ikulu) | • ZONE I Makazi 8,000/= Makazi na Biashara 8,500/= <br> • ZONE II Makazi 6,000/= Makazi na Biashara 7,500/= <br> • ZONE III Makazi 3,000/= Makazi na Biashara 5,500/= |

**NB: Malipo yote yafanyike ndani ya Siku 90 baada ya kupata hati ya madai.**

***Kwa mawasiliano zaidi piga simu namba 0714 785513.***

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji,**
**DODOMA**

215542002


# JPM: Mafisadi bado wapo, tutawakamata

**Na Waandishi Wetu,** MWANZA

RAIS John Magufuli amesema mafisadi katika serikali ya awamu ya tano bado wapo, na kwamba ataendelea kuwashughulikia mpaka watapike fedha zote.

Rais Magufuli alitoa kauli hiyo jana, jijini Mwanza, katika hafla ya kuweka jiwe la msingi katika ujenzi wa meli mpya ya kisasa, chelezo na ukarabati wa meli ya Mv Victoria na Mv Butiama.

Alisema miradi hiyo ilicheleweshwa kwa kipindi kirefu kutokana na fedha kutafunwa na mafisadi.

"Ni lazima tuzungumze ukweli, kwamba ni lazima tufanye mabadiliko ya kweli kusaidia nchi yetu, kwa nini tuweze sasa na kwa nini ishindikane miaka yote hiyo?" Alihoji Rais Magufuli.

Akizungumzia ujenzi wa meli mpya, Rais Magufuli alisema zaidi ya miaka 20 baada ya kuzama kwa meli ya Mv Bukoba ilitakiwa kujengwa meli nyingine, lakini jambo hilo halikufanyika.

"Kama mnavyofahamu baada ya kuzama kwa Mv Bukoba kumekuwa na tatizo kubwa la usafiri kwa wanaozunguka Ziwa Victoria, nilipokuja katika kipindi cha uchaguzi mwaka 2015 niliahidi kununua meli na sikujua pesa nitatoa wapi."

"Niliwaza kwamba kama wengine wote waliopita hawakununua, mimi nitawezaje, lakini kumbe inawezekana, pesa zipo nyingi ila zinachezewa na mafisadi ambao hata sasa wapo, hawajaisha."

"Hivi sasa tunafanya mpango wa kujenga pia standard gauge (reli ya kisasa) kutoka Mwanza hadi Isaka, sasa msiniulize pesa nitatoa wapi, nitaendelea kubanana na mafisadi mpaka watapike zote."

INAENDELEA UK. 8

HABARI KITAIFA

# Vigogo wamlilia Ali Mufuruki

**Na Gwamaka Alipipi**

MFANYABIASHARA maarufu nchini, Ali Mufuruki (60), amefariki dunia akiwa Afrika Kusini alikokuwa akipatiwa matibabu, huku vigogo serikalini, wanasiasa na jumuiya ya wafanyabiashara wakimlilia.

Taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti wa Jukwaa la Maofisa Watendaji Wakuu wa kampuni (Ceo Roundtable - Ceort), Sanjay Rughan, ilieleza kuwa kabla ya kupelekwa Afrika Kusini kwa matibabu, Mufuruki alikuwa akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Aga Khan.

Mufuruki aliwahi kushika nafasi mbalimbali wakati wa uhai wake kama Mwenyekiti na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Infotech Investment Group, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Mawasiliano ya Simu za Mkononi ya Vodacom Tanzania kabla ya kujiuzulu nafasi hiyo Novemba 18, mwaka huu.

Pia alikuwa mwenyekiti mwanzilishi wa Mwenyekiti wa Kampuni ya Mwananchi Communications Ltd.

Wakati wa uhai wake, Mufuruki pia aliwahi kuandika kitabu kiitwacho "Safari ya Tanzania katika uchumi wa viwanda, 2016-2056: Kutoka kilimo hadi taifa lenye viwanda vya kiasa katika kipindi cha miaka 40."

**VIONGOZI WAMLILIA**

Rais John Magufuli kupitia akaunti yake ya mtandao wa kijamii wa Twitter alisema: "Nimehuzunishwa na taarifa za kifo cha rafiki yangu, Ali Mufuruki (Mwenyekiti na Mwanzilishi wa Ceort). Nitamkukumbuka kwa uzalendo na mchango wake katika kukuza sekta ya biashara na ushauri kwa serikali. Inna lillahi wa inna ilayhi raji'un".

Naye Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, kwenye akaunti yake ya mtandao wa Twitter aliandika: "Nimeshtushwa na kuondokwa kwa ghafla kwa mwenzetu Ali Mufuruki, mchango wako na mawazo yake katika jamii ya wafanyabiashara tutaukumbuka, ujumbe wako wa simu ulioniandikia Novemba 15, 2019 ulikuwa mzuri "Mh, approval za TASAC zimetoka nyingi sana leo. Nashukuru kwa Intervention yako muhimu". R.I.P".

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, alisema: "Natoa pole kwa familia ya marehemu Ali Mufuruki, Watanzania wote, wafanyabiashara na wawekezaji kwa kuondokewa na mpendwa wetu. Tutamkumbuka daima kwa mchango mkubwa alioutoa katika sekta ya biashara na uwekezaji. Hakika tumepoteza jemedari. Mwenyezi Mungu amrehemu."

Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) nayo ilieleza kuwa: "Hakuna neno maalum litakaloelezea huzuni zetu, kwa niaba ya jumuiya ya wafanyabiashara tunatuma salamu zetu za rambirambi kwa familia ya Ali Mufuruki katika kipindi hiki kigumu."

Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, alisema Mufuruki wakati wa uhai wake alitoa mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta binafsi. Mshauri Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, alisema: "Nimepokea kwa huzuni, masikitiko makubwa ya taarifa za kifo cha Ali Mufuruki kilichotokea jana katika Hospitali ya Morningside, Johannesburg Afrika Kusini, Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi. Amina. Hakika sisi ni wa Mungu na kwake yeye tutarejea."

# Serikali yakusudia kushusha gharama kuunganisha umeme

**Na Zuena Msuya**

NAIBU Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, amesema serikali inaangalia uwezekano wa kufanya tathmini ya kupunguza bei ya kuunganisha umeme kwa wateja wa miji na manispaa ili huduma hiyo iweze kumfikia kila mmoja na kuondoa malalamiko.

Mgalu alisema hayo mwishoni mwa wiki baada ya kubaini changamoto zilizoibuliwa na wawekezaji na wafanyabiashara katika mkutano wa mashauriano baina ya serikali, wawekezaji na wafanyabiashara, uliyofanyika katika mikoa ya Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.

Alieleza kuwa changamoto kubwa iliyokuwa ikizungumzwa katika sekta ya nishati kwenye mikutano hiyo ni pamoja na tofauti kubwa ya bei ya kuunganisha umeme kwa wateja waliopo katika vijiji, miji na manispaa kuwa haziendani na mazingira halisi ya eneo husika.

Alisema wafanyabiashara na wawekezaji wengi wamedai kuwa pamoja na serikali kuweka kiwango cha bei ya chini cha Sh. 27,000 kwa kuunganishiwa umeme vijijini, wanatozwa kiwango kikubwa kwa madai kuwa wapo katika maeneo ambayo hayakupitiwa na mradi wa usambazaji umeme vijijini REA pamoja na kuwa wapo vijijini.

Vile vile, alisema serikali inatambua hali hiyo na kwamba inaangalia jinsi ya kupunguza gharama ya kuunganisha umeme hadi maeneo hayo ya majiji na manispaa, ili kila mwananchi apate huduma hiyo kwa urahisi na kwa bei nafuu.

Kwa mujibu wa Mgalu, endapo bei ya kuunganisha umeme katika majiji na manispaa itashuka, pia baada ya kukamilika kwa mradi wa kufua umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji wa Julius Nyerere utakaozalisha zaidi ya megawati 2000 za umeme pia gharama ya kununua umeme itashuka.

Aliwaeleza wafanyabiashara na wawekezaji wenye changamoto za umeme katika maeneo yao kufika wizarani kwa ajili ya kutatuliwa changamoto hizo kwa kuwa nishati ya umeme ni moyo wa uchumi na bila umeme hakuna viwanda.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA (TASAC)

MIAKA 58 YA UHURU WA TANZANIA 1961-2019

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania yaani "Tanzania Shipping Agencies Corporation (TASAC)", tunampongeza Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wote kusherehekea miaka 58 ya Uhuru wa Tanzania.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu akupe afya njema, hekima na busara za kutuongoza kwa upendo, amani, umoja na utulivu ili tuijenge nchi yetu.

MUNGU IBARIKI TANZANIA



*Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli*
*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

**Barua Pepe:** info@tasac.go.tz / customercare@tasac.go.tz/
**Tovuti:** www.tasac.go.tz

215548502

## CCM yawatumbua vigogo halmashauri

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KIKAO cha Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Morogoro, kimewavua uongozi Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, Furaha Lilongeri na makamu wake, Amina Seif pamoja na wajumbe saba wa kamati ya mipango na fedha wa halmashauri hiyo.

Katibu wa CCM Mkoa wa Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, alisema uamuzi huo ulifikiwa na wajumbe wa kamati hiyo kwa maslahi ya chama hicho, na kwamba waliovuliwa nyadhifa hizo watabaki kutumikia katika nafasi zao za udiwani.

Alisema Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Morogoro imejiridhisha kuwa viongozi waliovuliwa uongozi wameshindwa kusimamia dhamana waliyopewa na wananchi na chama, pamoja na kukiuka maadili ya uongozi.

"CCM Morogoro tumemwelewa Rais John Magufuli anachotaka, tumeamua kuanza kusafisha nyumba yetu, hivyo tumewavua uongozi mwenyekiti na makamu wake wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga lengo ni kuonyesha tofauti za kifikra, kimtazamo na tafsiri hasi inayotolewa na upinzani," alisemaShaka.

Akizungumzia hilo uamuzi huo, Lilongeri, alisema alishaandika barua ya kujiuzulu nafasi hiyo kwa ajili ya kupisha uchunguzi kabla ya maamuzi hayo kufanyika, na kwamba amebaki kutumikia nafasi ya udiwani Kata ya Mwaya.

Mapema Septemba Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alifanya ziara katika mkoa wa Morogoro na kubaini ubadhirifu mkubwa wa fedha za serikali, hivyo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ulanga aliondolewa na kuagiza watumishi wote waliohusika wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Kutokana na hali hiyo, CCM ilimwahidi Majaliwa kuwa haitasita kuchukua hatua dhidi ya viongozi wake waliohusika.



Watoto wakiwa kwenye matembezi ya hisani mwishoni mwa wiki yaliyoandaliwa na Shirika la Time To Help kwa ajili ya kusaidia watoto wenye ulemavu wa viungo na akili wanaolelewa kwenye kituo cha Baba Oreste Bunju B jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 698 washinda rufani mikopo vyuo vikuu

**Na Maulid Mmbaga**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imetangaza orodha ya majina 698 ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza watakaopata mikopo baada ya kushinda rufani zao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na bodi hiyo kwenye tovuti yake, wanafunzi hao ni wale waliofanikiwa kupitia dirisha la rufani kufuatia kukosa au kupata kiwango kidogo cha mikopo awamu nne zilizopita.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa wanafunzi hao wamepangiwa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 2.46, na kufanya jumla ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza waliopata mikopo hadi sasa kufikia 49,485.

Aidha, bodi hiyo imeahidi kutoa taarifa ya kina ya utoaji wa mikopo kwa mwaka wa masomo 2019/2020 itatolewa wiki ijayo baada ya uchambuzi wa mwisho kukamilika.

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema kuhusu viwango walivyopangiwa vinapatikana katika akaunti zao binafsi walizotumia kuomba mikopo.

"Tumeshaweka taarifa za wanafunzi katika mfumo, hivyo kila mmoja anatakiwa kuingia katika akaunti yake ya kuona taarifa zake ambazo pia zitatumwa vyuoni," alisema Badru.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, HESLB, imeboresha mifumo yake na wanafunzi wa mwaka wa kwanza walioomba mikopo wanaweza kuona taarifa zinazowahusu popote walipo kupitia simu zao.






# Faini 300,000/- wasiopeleka shule waliochaguliwa kidato cha kwanza

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

SERIKALI mkoani Katavi imeagiza kukamatwa na kisha kutozwa faini ya Sh. 300,000 au kwenda jela miezi miwili wazazi ambao watoto wao wamechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza Januari 2020 na kushindwa kuwapeleka shule.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera, wakati akizungumza katika kikao cha bodi ya uchaguzi wa wanafunzi watakaojiunga kidato cha kwanza mwakani baada ya kuhitimu na kufaulu mitihani yao.

Aliagiza kuwa wanafunzi wote waliopangiwa kujiunga kidato cha kwanza ambao watashindwa kwenda shule wazazi wa watoto hao ni lazima wakamatwe na watozwe faini ya Sh. 300,000 au kwenda jela kutumikia kifungo cha miezi miwili.

Alisema mkoa huo utaanzisha mahakama zinazotembea kwa ajili ya kuwahukumu wazazi wa watoto ambao watakuwa wameshindwa kuripoti shule na watahukumiwa huko huko waliko.

Aliagiza pia hataki kusikia katika mkoa huo kuna mwanafunzi anasoma akiwa amekaa chini kwani watakuwa hawamtendai haki Rais John Magufuli aliyeanzisha utaratibu wa elimu bila malipo.

Aliwataka wakuu wa wilaya zote za mkoa huo kushirikiana na serikali za vijiji zenye hifadhi za misitu pamoja na wakala wa misitu TFS ili watoe kibali cha kuvuna mbao kwa ajili ya kutengeneza madawati kwenye shule ambazo zitakuwa na upungufu wa madawati.

Aliwaonya baadhi ya wazazi ambao wamekuwa na tabia ya kutaka watoto wao kwenda shule ili waolewe waache tabia

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# Bodi yaondoa hofu wakulima wa pamba

**Na Happy Severine,** MEATU

BODI ya Pamba imewatoa hofu wakulima wa zao la pamba katika Wilaya ya Meatu mkoani Simiyu, kuhusu upatikanaji wa mbegu kuelekea msimu mpya wa kilimo ambao umeshaanza.

Akizungumza na wakulima wa zao hilo katika vijiji vya Isengwa na Mwandoya wilayani humo pamoja na kamati ya mazao ya wilaya, Mkaguzi wa pamba wa Bodi hiyo Wilaya ya Meatu, Jeremiah Kalissa, alisema mbegu zipo za kutosha.

Alisema bodi itahakikisha kila mkulima mwenye kuhitaji kulima pamba anapatiwa mbegu za kutosha eneo lake la kilimo hata kama hatakuwa na uwezo wa kununua.

Kalissa alisema jumla ya kampuni sita za pamba zimepewa kazi ya kusambaza mbegu kwa wakulima, ambapo kati ya tani 2,290 zinazohitajika kwenye wilaya hiyo, tani 1,850 zimesambazwa kwa wakulima.

Alisema ndani ya wiki moja mbegu nyingine ambazo hazisambazwa zitakuwa tayari zimewafikia wakulima, kwa kuwa baadhi ya kampuni zinaendelea kupakia mbegu hizo. "Bodi tumejipanga kuhakikisha kila mkulima anapata mbegu za kutosha, serikali imeagiza mkulima hata kama hatakuwa na pesa za kununua mbegu, akopeshwe na baada ya mavuno atakatwa," alisema Kalissa.

Alisema awali mahitaji ya mbegu kwenye wilaya hiyo yalikuwa tani 2,100, ambapo mahitaji yameongezeka tani 190 na kueleza kuwa wakulima wote watapewa mbegu haraka na kwa wakati.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Joseph Chilongani ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mazao, aliwataka wakulima kuwa wakweli katika kuchukua mbegu hizo kulingana na maeneo yao ya kilimo.

Alisema baadhi ya wakulima wamekuwa wakidanganya kwa kutaka mbegu nyingi kuliko uhalisia wa meneo yao, na kwamba wamekuwa wakiziuza kwa bei kubwa na wakati mwingine kuzifanya kuwa malisho ya mifugo yao.

# TRA yang'ara tuzo NBAA

**Na Veronica Kazimoto**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imeshinda tuzo mbili ikiwamo mshindi wa jumla katika uandaaji bora wa taarifa za hesabu mwaka 2018 kwa kufuata viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma (IPSASs).

Katika hafla ya utoaji wa tuzo hizo iliyofanyika katika Kituo cha Mikutano cha NBAA, Bunju jijini Dar es Salaam, TRA imeibuka mshindi wa kwanza katika uandaaji bora wa taarifa za hesabu kwenye kipengele cha Wakala wa Serikali na mshindi wa jumla kwa taasisi, wakala, kampuni na mashirika mbalimbali ambayo yamefanya vizuri katika kuandaa taarifa za fedha katika shughuli zao za kila siku.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hizo, Kamishna Mkuu wa TRA, Dk. Edwin Mhede, ameipongeza Idara ya Fedha na nyingine ndani ya mamlaka hiyo kwa kufanikisha upatikanaji wa tuzo hizo.

"Nachukua nafasi hii kumshukuru Mkuu wa Idara anayehusika na Idara ya Fedha pamoja na wakuu wa idara nyingine ndani ya mamlaka maana zote zinatoa mchango mkubwa kuhakikisha idara hii inatoa taarifa sahihi na zenye kuleta mipango sahihi kwa mamlaka na serikali kwa ujumla," alisema Dk. Mhede.

Dk. Mhede alieleza kuwa, taarifa sahihi ni msingi wa mipango kwa kuwa taasisi isiyopanga kushinda ni sawa na taasisi inayopanga kushindwa hivyo suala la uandaaji bora wa taarifa za hesabu ni moja ya ufanisi wa ofisi yoyote hapa ulimwenguni. Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (NBAA), ndiyo hutoa tuzo hizo kila mwaka na mwaka 2017, TRA iliibuka mshindi wa kwanza tena katika uandaaji bora wa taarifa za hesabu katika kipengele cha Wakala wa Serikali.

# Serikali kukuza sekta viwanda, biashara

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imeweka mkakati kuhakikisha inaboresha na kuikuza sekta ya viwanda na biashara nchini ili kuinua kipato cha Watanzania.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Tanzania, Stella Manyanya, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya uzinduzi wa maonyesho ya nne ya bidhaa zinazozalishwa nchini, yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema Tanzania kuna asilimia tatu ya viwanda vikubwa, na 97 vidogo, na kwamba kuna uhaba wa uzalishaji wa bidhaa zenye ubora.

Alisema hali hiyo inasababishwa na tatizo la uhaba wa wataalamu wa kuzalisha bidhaa zenye ubora kwenye viwanda vya nchini.


"Wafanyabiashara wenye viwanda wajitahidi kuzalisha bidhaa zenye ubora zitakazoshindana na mataifa mengine katika soko la kimataifa," alisema Manyanya na kuongeza:

"Tanzania tuna fursa ya malighafi nyingi hivyo tuzitumie kikamilifu ili kuinua uchumi wa viwanda nchini."

Vile vile, alisema serikali inafanya jitihada kuzuia bidhaa feki kuingia nchini na kuhakikisha soko linakuwa na zenye ubora. Kuhusu maonyesho hayo, alisema idadi ya washiriki imeongezeka kutoka 413 mwaka jana hadi kufikia 540 mwaka huu. Awali Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya chombo cha serikali chenye mamlaka ya udhibiti, utendaji na usimamizi wa biashara Tanzania (TanTred), Dk. Ng'wanza Kamata, alisema agenda ya viwanda itakua endelevu nchini.


TANZANIA SOCIAL ACTION FUND
MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII


MAADHIMISHO YA MIAKA 58 YA UHURU



**Marehemu Julius K. Nyerere**
Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**1961 - 1985**




**Mhe. Ali H. Mwinyi**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**1985 - 1995**



**Mhe. Benjamin W. Mkapa**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**1995 - 2005**



**Mhe. Dkt Jakaya M.Kikwete**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**2005 - 2015**



**Mhe. Dkt John P. Magufuli**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**2015 -**

Bodi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF tunaungana na Watanzania kukupongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli** kwa kuadhimisha **miaka 58 ya Uhuru wa Tanzania Bara**

***"TASAF itaendelea kuunga mkono jitihada za serikali yako katika kupambana na umaskini".***

*Pamoja Tuondoe Umaskini*

Mkurugenzi Mtendaji
**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF**
Barabara ya Jakaya Mrisho Kikwete
S.L.P 2719, Dodoma, Tanzania
Simu: **+255 26 296 3866**, Nukushi: +255 26 296 3871,
Barua pepe: **info@tasaf.go.tz**, Tovuti: **www.tasaf.go.tz**

215548402

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kongole Simba kwa hili la kituo cha afya

**KLABU** ya Simba imekamilisha awamu ya kwanza ya mradi wake wa ujenzi wa viwanja viwili vya mazoezi katika eneo la Bunju jijini Dar es Salaam na Jumamosi ilivikabidhi kwa mashabiki na wanachama wao.

Viwanja hivyo ambavyo ni cha nyasi bandia na asili, tayari vinaweza kuanza kutumika na klabu hiyo imeelezwa inaweza kuanza kuvitumia rasmi kuanzia leo.

Hakika hiyo ni hatua ya kupongezwa kwani ni miaka 83 sasa tangu klabu hiyo ilipoanzishwa mwaka 1936 na imekuwa ikifanya mazoezi katika viwanja vya kukodi, lakini sasa imetoka huko na inamulika mbele zaidi.

Kwa mujibu wa uongoziwa klabu hiyo, wamekuwa wakitumia kiasi cha Sh. 300,000 hadi 500,000/- kila siku kwa ajili ya kukodi tu viwanja vya kufanyia mazoezi.

Kwa mantiki hiyo, Simba ilikuwa ikitumia si chini ya Sh. milioni tisa kwa ajili ya kukodi tu viwanja vya kufanyia mazoezi ambazo wanakwenda kuzioko kufuatia kukamilisha viwanja vyake vya mazoezi Bunju.

Hata hivyo, mradi huo ambao umetekelezwa na Mwekezaji wao, Mohamed "Mo" Dewji kwa zaidi ya asilimia 90, lengo la kukabidhiwa kwa mashabiki na wanachama wa klabu hiyo ni ili sasa kuwataka kuunganisha nguvu kuweza kuchangia kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa matofali na mambo mengine.

Hivyo, ni wakati sasa kwa wanachama, mashabiki na wapenzi wa timu hiyo kuunganisha nguvu ili kuweza kufikia malengo hayo na wote kuwa sehemu ya mafanikio ya klabu hiyo ambayo imeingia katika mfumo wa uendeshwaji wa hisa.

Mbali na hatua hiyo Simba iliyofikia, imeeleza mradi huo ni sehemu tu kati ya miradi mingine mikubwa wanayotarajia kuitekeleza katika eneo hilo la Bunju.

Mradi mwingine unaoelezwa kutarajiwa kufanywa katika eneo hilo ambalo tayari pia ujenzi wa vyumba vya kubadilishia kwa wachezaji umekamilika, ni hosteli ya kisasa kwa ajili ya timu ya wakubwa na ile ya vijana ambao utaanza mara moja huku Mo akiahidi kuchangia Sh. milioni 500 kati ya bilioni mbili zinazohitajika ili kuukamilisha.

Lakini kubwa kuliko yote ambalo limelifurahisha Nipashe ni mpango wa ujenzi wa kituo cha afya katika eneo hilo ulioelezwa na Mjumbe wa Kamati ya Utendaji wa klabu hiyo, Asha Baraka wakati wa kutambulisha viwanja hivyo kwa wanachama na mashabiki juzi.

Kwa mujibu wa mjumbe huyo, klabu hiyo imeona kuna haja ya kujenga kituo cha afya katika eneo hilo, na si tu kwa ajili ya kuleta karibu huduma ya matibabu kwa wachezaji wao bali kurejesha huduma kwa jamii kwa kuwahudumia wakazi walio jirani na uwanja huo.

Haya ndiyo maendeleo Nipashe inayotamani kuona yakitokea katika soka letu, na tunaamini hatua hiyo itaigwa na klabu nyingine za Tanzania ambazo zinatamani kufikia mafanikio hayo.

Tunatumai kuona pia hilo likifanyika kwa Azam katika Uwanja wao wa Chamazi na klabu nyingine, lakini pia likiingizwa kwenye mipango ya Yanga ambayo imepewa eneo la kujenga uwanja Kigamboni nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Lengo letu ni kuona Watanzania hawaishii tu kutumia fedha zao kwa ajili ya kulipa viingilio uwanjani, bali pia wakinufaika kwa kupata huduma za kijamii kama hiyo ya kusogezewa kituo cha afya karibu kutoka kwa klabu hizo.

Mwisho tunaiomba Simba na klabu nyingine nchini ziendelee kubuni miradi ambayo kwa namna moja ama nyingine itanufaisha na jamii inayoizunguka katika maeneo husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwango

# Mfumo wa Kombe la Chalenji ubadilishwe

**MICHUANO** ya Kombe la Chalenji kwa wanaume kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (Cecafa) inaendelea kutimua vumbi nchini Uganda, Tanzania Bara ikiwakilishwa na Kilimanjaro Stars, upande wa pili wa Muungano ukiwakilishwa na Zanzibar Heroes.

Ni michuano ambayo bila kupepesa macho ni kwamba kadri siku zinavyozidi kusonga mbele inaonekana kupungua msisimko wake.

Cha ajabu ni kwamba wakati michuano hiyo kwa upande wa wanaume msisimko wake umepungua, lakini umehamia kwa Chalenji ya Wanawake.

Tuliona hivi karibuni michuano hiyo iliyofanyika nchini kwenye Uwanja wa Azam Complex, ambapo mbali na kandanda safi la kuvutia kwa wanawake, tumeshuhudia idadi kubwa ya mashabiki ikihudhuria bila kujali mvua wala jua.

Kwa upande wa wanaume michuano hii inapungua msisimko nadhani kutokana na muundo wake bado ni wa kizamani na haijafanyiwa marekebisho ili kuendana na mtazamo wa kisasa.

Kwa miaka mingi sasa michuano hiyo inaendeshwa kwa mtindo wa timu kukusanyika kwenye kituo kimoja na kuchezwa kwa muda wa wiki mbili.

Mfumo huu ambao unatumika pia kwenye michuano ya Kagame Cup unaonekana umepitwa na wakati na Cecafa inatakiwa ikae kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kubadilisha mfumo kuendana na wakati.

Ukiangalia hata huko nyuma, hata mfumo huu unaotumika sasa ulibadilishwa, hivyo kumbe inaonekana kabisa kuna uwezekano wa watu kukaa na kuangalia mfumo mbadala.

Zamani kabla ya mfumo huu wakati huo zikishiriki timu nne, hakukuwa na robo, nusu fainali au fainali, badala yake timu zilikuwa kundi moja na kucheza kwa mfumo wa ligi, inayokuwa na pointi nyingi ndiyo bingwa.

Nchi wanachama zilivyokuwa zikiongezeka ndipo mfumo ulipobadilishwa na kuwekwa makundi, huku timu mbili za juu zikitinga hatua ya nusu hadi fainali na zilipokuwa zinazidi kuongezeka ilifika hatua mtoano unaanzia robo fainali hadi fainali.

Ingeweza kuwa hata msimu huu hivyo, lakini kutokana na Ethiopia, DR Congo, Rwanda na Sudan Kusini kujitoa, makundi yamebaki mawili tu, hivyo kila kundi litatoa washindi wawili zitakaingia nusu fainali.

Ni wakati sasa wa Cecafa kubadilika na kuweka mfumo mpya kama ambavyo tayari nchi za Ulaya zimeanza kufanya.

Michuano kama hii sasa ingeweza kabisa kuchezwa kwa mtindo wa nyumbani na ugenini ili kuepusha ligi kusimama, lakini kuifanya kuwa na mvuto zaidi.

Mfano kwa makundi yaliyopo sasa timu hizo zingekuwa zikisubiri Kalenda ya Fifa ndipo ziwe zinacheza na hiyo kuifanya michuano hiyo endelevu, badala kuwa ya wiki mbili tu.

Ni mfumo ambao unaweza kutumika hata kwenye michuano ya Kagame Cup ili kuipa thamani michuano ya Cecafa na kuzipa nguvu klabu zake pamoja na wachezaji kucheza mechi nyingi.

Cecafa ingeweka mechi za fainali tu kuwa iwe moja tena iwe inachagua nchi na uwanja wa kucheza fainali mapema kabisa wakati wa droo, lakini makundi, robo na nusu fainali ingekuwa inachezwa nyumbani na ugenini.

Ikifanya hivi, inawezekana kabisa michuano hii ya kwa upande wa wanaume kwa timu za taifa na Kagame Cup kwa klabu ikarejesha mvuto na msisimko wake wa miaka ya '80 hadi katikati ya '90, lakini hii ya kuzikusanya timu sehemu moja, imepitwa na wakati.

## HABARI KITAIFA

# Mfanyakazi atuhumiwa kumwibia bosi hati ardhi, akopea

**Na Hassan Mabuye,** IRINGA

KATIKA hali isiyokuwa ya kawaida, mkazi wa Iringa mjini, Lugano Mwadini, amenusurika nyumba yake kupigwa mnada baada ya kijana wake wa kazi kumtuhumu kumwibia hati ya umiliki wa ardhi na kukopa Sh. 1,000,000. Tukio hilo lilibainika katika mkutano wa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, kupitia programu yake ya 'Funguka kwa Waziri' mkoani Iringa alipokuwa akisikiliza na kutatua kero za ardhi kwa wananchi wa mkoa huo.

Lugano alimtuhumu kijana wake wa kazi kumwibia hati na kuenda kukopa kwa Laurence Panklas, ambaye ni askari wa Jeshi la Polisi mkoani humo anayekopesha kwa riba ya 400,000, kila mwezi ambazo kijana huyo hakuweza kuzirudisha kwa wakati jambo lililosababisha kutaka kuuzwa kwa nyumba ya bosi huyo ili kufidia deni hilo.

Lugano alibaini hilo baada ya kupigiwa simu na mkopeshaji huyo kumtaka kwenda kubadilisha umiliki wa hati hiyo ili apewe mtu mwingine kwa kuwa hati yake imekopewa na inadaiwa Sh. 1,400,000.

"Mimi nilikuwa sipo, lakini nikaja kupata taarifa kwa kupigiwa simu kwamba kijana wangu wa kazi ameniibia hati yangu wakati nikiwa katika kazi zangu na amekopea kwa askari mmoja ambaye anakopesha kwa riba ya laki nne kila mwezi, kwa hiyo kijana wangu anadaiwa 1,400,000 na hajalipa hadi sasa," alisema Lugano.

Waziri Lukuvi alimwagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, kushughulikia suala hilo kwanza kwa askari wa Jeshi la Polisi ambaye anafanya biashara ya pesa na kama ana kibali cha biashara hiyo na analipa kodi, na kama halipi alipe kodi kwa miamala yote aliyowahi kufanya.

Kadhalika, aliagiza kukamatwa kwa kijana wa kazi ili alipe deni hilo kwa bosi wake na kueleza sababu za kufanya wizi huo.

Katika mkutano huo Waziri Lukuvi alisikiliza na kutatua migogoro ya wakazi wa mkoani Iringa takribani 200 kwa siku moja, huku baadhi ya wananchi wakieleza kuridhishwa kwa juhudi za Lukuvi kusikiliza na kutatua migogoro ya ardhi ya wakazi wa maeneo mbalimbali nchini bila kubagua.

## Chadema yapitisha wagombea mabaraza

INATOKA UK. 2

Walioteuliwa kugombea uenyekiti wa baraza hilo Taifa ni Mathayo Philipo Gekul, John Justin Pambalu na Dorcas Francis Mwilafi, huku kwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti akiteuliwa Mohonia Joseph, Elizabeth Pius Kasera, Ester Musa Fulano, Mozza Ally Mushi na Francis Garatwa kwa upande wa bara na Rukia Abubakar Mohamed na Omar Nassoro kwa upande wa Zanzibar.

Alisema kigezo kingine kilichozingatiwa ni suala la maadili ambapo mwenendo katika mitandao ya kijamii ya wagombea wote walioomba nafasi za uongozi ilichunguzwa, na waliobainika kuwa na utovu wa maadili katika mitandao hiyo waliengulliwa.

Kwa upande wa Baraza la Wanawake (Bawacha), Mbunge wa Kawe, Halima Mdee ndiye pekee atakayewania nafasi ya uenyekiti, huku Hawa Mwaifunga na Aisha Luja wakipishwa kugombea nafasi ya makamu mwenyekiti.

Kwa upande wa Baraza la Wazee Kamati Kuu ya chama hicho imewapitisha Hashimu Juma Issa na Hugho Samali Kimaryo kuwania nafasi ya uenyekiti, huku Mbunge wa Viti Maalum, Suzan Lyimo akipitishwa kuwania nafasi makamu mwenyekiti bara wa baraza hilo, Mwanamrisho Abama na Idrissa Mkila wakipishwa kuwania nafasi ya makamu mwenyekiti upande wa Zanzibar.


MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA

MIAKA 58 YA UHURU



**Mh. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa
**MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA (TPA)**
wanaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**
na Wafanyakazi wote katika kuadhimisha
miaka 58 ya Uhuru wa Tanzania

**"HAPA KAZI TU"**

S.L.P 9184 DAR ES SALAAM BANDARI TOWER ONE STOP CENTRE
+255 22 2110401/5; + 255 22 2110371/5; +255 22 2137631/2
Namba za bure 0800 110032, 0800110047, Tovuti: www.ports.go.tz

tanzaniaportshq
tanzaniaportshq
TPAHQ
tanzaniaportshq

**Bandari ni Lango la Biashara Kitaifa na Kimataifa**

215547202

# DC aamuru bendera za upinzani kushushwa

INATOKA UK. 2

"Ninawaagiza wenyeviti hakikisheni mnakwenda kuzing'oa bendera zote za Chadema (Chama cha Demokrasia na Maendeleo) pamoja na za vyama vingine, sitaki kuziona zikipepea kwenye nyumba ya mtu yeyote, na atakayebisha tutamkamata na kumfungulia shtaka la kusababisha uchafu, na atakwenda jela mwezi mmoja au kulipa faini ya Sh. 50,000," alisema.

Sambamba na maagizo hayo, aliwaagiza wenyeviti hao kuhakikisha hata kwenye mpango wa kusaidia kaya maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) wanawaondoa wale wote ambao ni wanufaika wanaunga mkono vyama vya upinzani.

Mkuu huyo wa wilaya aliwataka wenyeviti hao kwenda kutatua changamoto za wananchi ikiwamo migogoro ya ardhi, kuimalisha ulinzi na usalama katika maeneo yao, kudhibiti suala la watoto kuhamia mtaani pamoja na kusimamia ukusanyaji wa mapato.

**MSAJILI: SINA TAARIFA**

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi, alisema hawajapokea taarifa rasmi ya jambo hilo na wakipokea watakuwa kwenye nafasi nzuri ya kulizungumzia.

"Ndiyo kwanza nasikia kutoka kwako, hadi sasa hatujapokea taarifa rasmi ya jambo hilo, tukishapokea ndiyo tutazungumza," alisema.

**CHADEMA: TUNASUBIRI KAULI**

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Habari wa Chadema, Tumaini Makene, alisema wanasubiri kusikia kauli ya msajili juu ya jambo hilo kwa kuwa ndiye mlezi wa vyama vyote.

"Mara kadhaa tumemsikia Msajili akizungumza linapotokea jambo, na hili tunatarajia atazungumza kwa haraka, pia mamlaka iliyomteua DC huyo ichukue hatua dhidi yake kwa kuwa kauli hiyo utasababisha upotevu wa amani.

"Si sawa kwa jambo hili kuachwa litasababisha machafuko kwa kuwa vyama vipo kisheria na vimesajiliwa. Bendera zinapandishwa na viongozi na wanachama kwa mapenzi yao, wakiona wanabaguliwa watakuwa na haki ya kutoa hisia zao na hapo zitatokea vurugu," alisema.

**ACT-WAZALENDO WANENA**

Akizungumza na Nipashe, Katibu Mkuu wa ACT - Wazalendo, Doroth Semu, alisema jambo hilo halikubaliki, na kwamba viongozi wa kisiasa waelewe kuwa ni nchi ya vyama vingi na vyama vipo kisheria, hivyo ni haki kupeperusha bendera zake mahali zinaporuhusiwa.

"Mkuu wa wilaya kuzuia watu kupeperusha bendera na kuagiza zilizoko zishushwe ni kosa, anavunja sheria na amani, kwa kuwa wanachama ambao bendera zao zitashushwa hawatakubali na vurugu zitatokea... ni sahihi sisi kupeperusha bendera zetu kokote kunakostahili, viongozi wa siasa wanapaswa kuelewa mipaka na sheria za nchi katika utekelezaji wa majukumu yao," alisema.

**KAULI YA CUF**

Mkurugenzi wa Habari wa Chama cha Wananchi (CUF), Abdul Kambaya, alisema jambo hilo linaonyesha matumizi mabaya ya madaraka kwa kuwa DC anataka kumpendezesha anayechukia vyama vya upinzani au kujionyesha yeye ni kiboko wa vyama hivyo.

Alisema maamuzi hayo hayana tija na hayatampa utulivu wa kisiasa kiongozi huyo bali yatazua changamoto zaidi, na kwamba siyo jambo leye tija hasa kuelekea Siku ya Uhuru (leo).

"Kauli kama hizi zilitolewa na wakoloni, lakini miaka 58 ya Uhuru bado kuna mkuu wa wilaya ana fikra za ukoloni ambazo wenyewe wanajutia kauli zao, ni jambo la kusikitisha sana," alisema Kambaya na kuongeza:

"Kutoa kauli za ajabu kiasi hicho ndani ya taifa ni mbaya sana, busara imwongoze amshawishi mbunge wake apeleke hoja bungeni ya kufuta vyama vya upinzani kuliko yeye kuelekeza bendera zishushwe."

**Imeandikwa na Salome Kitomari (DAR) na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

# Afrika, EU kujadili mkataba wa EPA

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Mawaziri wa nchi za Afrika, Caribbean na Pacific (ACP), Tanzania ikiwamo zimekubaliana na Umoja wa Ulaya kufanya maridhiano katika maeneo yanayoonekana kuwa kikwazo kwa baadhi ya nchi hizo kutosaini mkataba wa Shirika la Kulinda Mazingira (EPA) ama kuitekeleza.

Nchi hizo zimefikia makubaliano hayo katika mkutano wa 110 wa nchi hizo unaoendelea Nairobi, nchini Kenya.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba John Kabudi, (pichani) alisema nchi hizo zimekubaliana kufanya mapitio mapya ya mikataba ya EPA uliyoingia na nchi za ACP.

Alisema kuwa mapitio hayo yanalenga kuzingatia hali halisi ya sasa duniani ikiwa ni pamoja na Malengo ya Dunia ya Maendeleo Endelevu (MDG), Makubaliano ya Mkataba wa Paris kuhusu mazingira na uhalisia mwingine ndani na nje ya Umoja wa Ulaya.

Maazimio mengine yaliyopitishwa katika mkutano huo ni pamoja na kuifanya ACP kuwa umoja wa kisasa zaidi katika malengo yake, muundo wake na mikakati yake katika kufikia ACP tunayoitaka (The ACP we want) ikiwa ni pamoja na kubadilisha jina kutoka Kundi la ACP na kuwa Umoja wa ACP.

Prof. Kabudi alisema lengo la mabadiliko hayo ni kuifanya ACP kuwa na nguvu zaidi katika kupanga, kuweka mikakati na kutekeleza kwa ufanisi malengo ya umoja huo.

Pia baraza limefanya uamuzi wa kumchagua Balozi George Rebelo Pinto Chikoti kutoka Jamhuri ya Angola kuwa Katibu Mkuu wa Sekretariati ya ACP kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025.

Kuhusu suala la kujitegemea baraza limeidhinisha uamuzi wa kuanzisha mfuko wa uwekezaji wa jumuiya ya kundi la nchi za Afrika Caribbean na Pasific kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya utegemezi katika kue-



ndesha jumuiya. Mfuko huu utaweza kufanya uwekezaji kwa kutumia fedha za umoja pamoja fedha kutoka katika vyanzo mbalimbali badala ya kutegemea zaidi ufadhili kutoka Umoja wa Ulaya.

## Faini 300,000/- wasiopeleka shule waliochaguliwa kidato cha kwanza

INATOKA UK. 4

hiyo mara moja kwani watakaobainika kufanya hivyo yeye kama mkuu wa mkoa atawachukulia hatua kali za kisheria.

Homera alisema wanafunzi wote waliomaliza darasa la saba na kufaulu watakwenda sekondari, na wale wasiofaulu watapangiwa kujiunga na vyuo vya ufundi hivyo hakuna mtoto atakaye kuwa akizurura ovyo mitaani.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi, Abdalla Malela, alisema mkoa huo unatarajia kukamilisha ujenzi wa shule saba za sekondari za kata ifikapo Januari 15 kitendo kitakachosaidia wanafunzi kuepukana na tatizo la kusoma katika shule zilizo mbali na makwao.

Alizitaja shule hizo za kata kuwa ni Sekondari ya Kasekese, Kakoso, Kakese, Itenka, Ugala, Senkwa na Ilunde.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Katavi, Newaho Mkisi, alisema jumla ya wanafunzi 8,510 wamechaguliwa kujiunga na shule za sekondari za kutwa wasichana wakiwa 4,281 na wavulana 4,229 na waliochaguliwa kujiunga na shule za bweni 31, wavulana 22 na wasichana tisa na wafunzi wanane wamechaguliwa kujiunga na shule zenye mahitaji maalum.

Alisema ufaulu wa wanafunzi kwa mkoa huo umeongezeka kwa asilimia 7.07 na kuufanya mkoa huo kupanda katika ufaulu wa kitaifa kutoka nafasi ya tisa ya mwaka jana hadi kuwa katika nafasi ya tano kitaifa mwaka huu.

Diwani wa Makanyagio, Haidari Sumry alisema idadi ya wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na shule za bweni kutoka katika mkoa huo ni chache, hivyo mkoa ungeangalia namna ya kuanzisha shule moja ya sekondari ya kutwa ambayo itakuwa ikiwachukua wanafunzi wenye ufaulu wa juu.

# JPM: Mafisadi bado wapo, tutawakamata

INATOKA UK. 2

Katika ujenzi wa meli hiyo na ukarabati wa Mv Victoria na Mv Butiama, Rais Magufuli alisema miradi hiyo kwa ujumla wake itagharimu Sh. bilioni 153 ambazo ni fedha za ndani.

Alizitaka mamlaka zinazohusika na usimamizi wa miradi hiyo, kuhakikisha kwamba inazalisha faida.

Alisema katika kipindi cha uongozi wake hataki kusikia chombo chochote kinachojiendesha kwa hasara. "Kwenye serikali yangu kitu kinachoitwa hasara ameshakufa zamani, kwangu mimi anayeishi ni faida tu, kwa hiyo nataka mhakikishe miradi hii yote inazalisha," alisema Rais Magufuli.

Pia aliagiza miradi hiyo kukamilika kwa wakati ili kusaidia kutatua tatizo la usafiri katika Ziwa Victoria.

"Nimeambiwa ukarabati wa chelezo umekamilika kwa asilimia 68, Mv Victoria asilimia 65 na Mv Butiama asilimia 60, hii inanipa uhakika kwamba miradi hii itakamilika kwa wakati uliopangwa na ikiwezekana hata kabla ya wakati ili kutatua tatizo la usafiri katika ziwa hili la Victoria," alisema Rais Magufuli.

Akizungumzia kuanza kwa safari za treni kutoka Dar es Salaam hadi Moshi mkoani Kilimanjaro, Rais Magufuli alisema ni jambo la kushangaza huduma hizo kisimama kwa kipindi kirefu.

"Na hii lazima tuzungumze ukweli, miaka 26 yote huduma za treni katika mkoa huo zilikuwa zimesimama. Siyo kwamba hakukuwa na pesa, isipokuwa hatukujipanga, hatukuona priority (kipaumbele) kwa pesa tunazokusanya kwa ajili ya maendeleo ya wananchi, huo ndio ukweli."

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), Eric Hamissi, alisema meli mpya itakuwa na madaraja matatu na kwamba ya kwanza itakuwa inabeba abiria 50, la pili abiria 316 na la tatu abiria 834.

Hamissi alisema itakuwa inafanya safari zake Mwanza, Bukoba, Musoma na nchi jirani za Kenya na Uganda.

Hamissi alisema, makandarasi wanaotekeleza miradi hii kwa upande wa ujenzi wa meli mpya ni Gas Entec akishirikiana na KANG NAM zote kutoka Korea ya Kusini pamoja na SUMA JKT ya Tanzania, ujenzi wa chelezo mkandarasi ni Stx Engine anashirikiana na SAE KYUNG zote za Korea Kusini, huku mkandarasi wa ukarabati wa meli za MV. Victoria na MV. Butiama ni KTMI nayo kutoka Korea ya Kusini. Katika hatua nyingine, Rais Magufuli aliwaagiza makandarasi wanaosimamia miradi hiyo kuhakikisha wanatekeleza miradi hiyo kwa ubora na ikiwezekana waikamilishe miradi hiyo kabla ya wakati.

"Wana-Mwanza jipangeni vizuri katika kuhakikisha miradi yote inayotekelezwa na serikali inawanufaisha, huku viongozi wote wa mikoa ikiwamo Mwanza kuhakikisha mnawahamasisha wananchi katika suala hilo," alisema.

**Imeandikwa na Elizabeth Zaya, Elizabeth Faustine na Neema Emmanuel, MWANZA**

## HABARI KITAIFA




Naibu Waziri Ofisa ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Josephat Kandege (katikati), akimkabidhi Wakala wa Mauzo, Masoko ya Fedha za Kigeni na Dhamana za Serikali wa Benki ya NBC, Erick Kabote, cheti cha kuhitimu mafunzo ya ulinzi kwenye masoko ya mitaji na dhamana yaliyotolewa na Mamlaka ya Mitaji na Dhamana (CMSA). Hafla hiyo ilifanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni kwa udhamini wa Benki ya NBC. Wa pili kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hiyo, Nicodemus Mkama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watakiwa kuwa karibu na wazalishaji, wasindikaji

**Na Felix Andrew**

MKUU wa Wilaya ya Mtwara, Evod Mmanda, amewataka watendaji wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuwafuatilia mara kwa mara wazalishaji wa bidhaa ili wakati wote wazalishe bidhaa bora na kuepukana na uwepo wa bidhaa hafifu sokoni.

Alitoa kauli hiyo wakati wa ufunguzi wa semina ya wazalishaji, wasindikaji na wauzaji wa bidhaa za chakula na vipodozi wa wilayani Mtwara.

Mmanda alisema imefika wakati sasa maofisa wa TBS watoke maofisini na kuwafuata wazalishaji kuwatafuta walipo, kuwaelimisha kupitia mitandao ya kijamii, redio, televisheni na magazeti, kuwaelekeza na kuwasimamia ili wazalishe bidhaa bora wakati wote.

"Tukiwafuatilia kwa karibu wazalishaji tutawasaidia kuendeleza ubunifu wao na hatimaye watafuata utaratibu wa kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozizalisha," alisema.

Alisema wajasiriamali ni kundi muhimu linalotoa mchango katika kuleta uhai na ustawi wa taifa la Tanzania hivyo mafunzo haya yatawawezesha kubadilishana uzoefu na elimu watakayoipata watawafikishia wengine ambao hawakupata fursa ya kupatiwa mafunzo.

Alisema elimu kuhusu matumizi ya viwango, udhibiti wa ubora, elimu ya vifungashio na usafi katika maeneo ya kazi pamoja na uelewa kuhusu taratibu za kisheria na kanuni zinazoongoza shughuli zinazofanywa ni muhimu kwa wazalishaji, wasindikaji na wauzaji wa bidhaa za chakula na vipodozi.

Aidha, Mmanda waliwataka wadau wa semina hiyo kuweka uzalendo mbele, uaminifu na uadilifu unahitajika katika uzalishaji na uuzaji wa bidhaa kwani kinyume chake, afya za watumiaji zitakuwa hatarini.

"Kama vyakula havina viwango vya kutosha, madhara yake ni makubwa, hivyo wasindikaji na TBS msaidiane kuliangalia suala hili kwa umakini," alisisitiza.

Alisema usindikaji wa bidhaa unapaswa kuwa katika viwango vinavyokubalika, mikakati na utafiti wa masoko unahitajika ili biashara iwe ya tija na kupanua wigo wa ajira nchini.

Naye Katibu Tawala wa Wilaya ya Lindi, Thomas Safari, akifungua semina mkoani Lindi kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo, Godfrey Zambi, alisema wazalishaji na wasindikaji wa bidhaa wanapaswa kuondokana na mazoea ya kuzalisha bidhaa bila ya kuzingatia viwango.

Alisema mkoa wa Lindi unazalisha chumvi kwa wingi, ingawa inasikitisha kuona kwamba wazalishaji wengi wanaiuza bila kuiongezea thamani kwa kuweka madini joto na kuthibitisha ubora wa chumvi, jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo ya wakazi wa mji wa Lindi.

Alisema umefika wakati sasa kwa wazalishaji wa chumvi kuthibitisha ubora ili kuongeza thamani ya bidhaa hiyo, na kuwauzia wananchi bidhaa iliyo bora.

# Taasisi, serikali za mitaa zabanwa uondoaji taka

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, George Simbachawene, amezitaka taasisi zote za umma na serikali za mitaa kuwa na mpango mkakati wa kisera, kikanuni na kimuundo katika uzoaji taka nchini.

Akifungua mdahalo wa udhibiti wa taka nchini ulioandaliwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwenye ukumbi wa Nkurumah mwishoni mwa wiki, Simbachawene alizitaka aliagiza taasisi zote za umma na serikali za mitaa kuhakikisha taka zote zinatolewa ama kurejelezwa kuwa malighafi ya kutengeneza vitu vingine.

Waziri huyo alirejea utafiti mbalimbali, akieleza kuwa wananchi wana utayari mkubwa katika kuchangia huduma za uzoaji taka.

"Kwa mfano, katika utafiti uliofanywa mwaka huu chini mradi wa Institutional for Inclusive Development, umeonyesha Mji wa Arusha, zaidi ya asilimia 90 ya wananchi huchangia gharama za huduma ya taka.

"Utafiti huo unaonyesha katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ni kati ya asilimia 70 na 80, Mji wa Dodoma asilimia 70 na Ilala asilimia 70 ya wananchi huchangia huduma husika.

"Udhibiti wa taka ngumu ni muhimu sana katika utunzaji wa mazingira na afya za viumbe hai kwa kizazi cha sasa na kijacho. Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 Kifungu cha 114 hadi 119, vinazungumzia masuala ya udhibiti wa taka ngumu," alifafanua.

Aliongeza kuwa kumekuwa na jitihada mbalimbali ambazo serikali kuu na halmashauri za miji na majiji kupitia serikali za mitaa zimetekeleza, ikiwa ni pamoja na kampeni za kuhakikisha hali ya udhibiti wa taka ngumu inamarika. Alizitaja baadhi ya kampeni hizo kuwa ni ushirikishwaji wa jamii kufanya usafi kila Jumamosi na ubinafsishaji wa shughuli za uzoaji taka kwa kutumia kampuni binafsi na vikundi vya kijamii (CBOs).

Alisema kampeni nyingine ni uanzishwaji wa kanuni za udhibiti wa taka ngumu za mwaka 2009 chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 na uanzishwaji wa kanuni za usimamizi wa mazingira za kupiga marufuku mifuko ya plastiki za mwaka 2019.

Awali, akimkaribisha Simbachwene aliyekuwa mgeni rasmi, Profesa Donata Tibuhwa wa UDSM, alisema chuo hicho kimeandaa mdahalo huo juu ya udhibiti wa taka na kuupa jina la 'Tanzania Bila Taka' kwa lengo la kuunga mkono jitihada za serikali kuhusu utunzaji wa mazingira.

Alisema wanaipongeza serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kufanikisha upigaji marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki nchini, akieleza kuwa mifuko hiyo ni mbali na kuwa hatari kwa mazingira, pia ni hatari kwa afya ya binadamu.

Mdahalo huo ulishirikisha pia wanafunzi na wadau mbalimbali wa masuala ya mazingira, wakiwamo wanaosimamia uondoaji wa taka.

# FCC kushughulikia biashara mtandaoni

**Na Juster Prudence**

TUME ya ushindani kwa kushirikiana na mamlaka za udhibiti nchini watachukua hatua kwa changamoto za biashara mtandaoni kiushindani, kutokana na kukithiri kwa upotoshaji na utapeli.

Akizungumza hivi karibuni katika maadhimisho ya siku ya ushindani yaliyoanza Desemba 3, mwaka huu, jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa tume hiyo, Prof. Humphrey Moshi wamejipanga vyema imejipanga kukabiliana na changamoto hizo.

Alizitaja changamoto hizo kuwa ni kukosekana kwa uaminifu, kuwepo kwa matangazo potofu, kukosekana kwa mfumo dhibiti wa kutatua malalamiko ya wateja na kukosekana kwa mfumo stahiki wa kuelimisha wateja kuhusu haki na wajibu wao kabla ya kufanya manunuzi mtandaoni.

Humphrey alieleza mipango ya tume kuwa ni kuunda mbinu bora za ushirikiano zitakazosaidia kutatua changamoto hizo kwa kuzingatia uzoefu uliopo duniani.

Naye Mkurugenzi Mkuu Tume ya Ushindani Bara, Geofrey Machimu, alisema tume imefanya kongamano na wataalamu wa sera na sheria ya ushindani ili kufanya tathmini kuhusu utekelezaji wa sera na sheria hizo.

Alisema pia watatoa ufafanuzi juu ya mpango wa muda mrefu wa miaka 15 Taifa limejipambanua kwamba mpango wa 3 wa miaka 5 utakua ni juu ya uchumi shindani.

Aidha, Mkurugenzi wa Tume ya Ushindani Zanzibar, Mohamed Jaffar, alisema kwa upande wa Zanzibar changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni kukosa weledi kwa kuwa tume ya ushindani nchini humo bado ni mpya.

Pia aliahidi kutoa elimu kwa watu juu ya ushindani wa kimtandao kwa mantiki ya kuwa wengi wanatumia nafasi hiyo kwenda kinyume kwa madai kwamba hawajui sheria.

# Msomi awataka vijana kidigitali

**Na Sabato Kasika**

VIJANA wametakiwa kuchangamkia fursa za kielimu, lakini wakizingatia zaidi elimu inayokwenda na wakati, ili wasibaki nyuma katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia.

Aidha, wametakiwa kuwa makini na kuelewa dunia inavyokwenda badala ya kusoma tu bali wafikiri mara mbili huku wakitambua kuwa kila kukicha mambo yanabadilika na yanakwenda kidigitali.

Wito huo ulitolewa juzi na Prof. Honest Ngowi wa Chuo Kikuu Mzumbe, tawi la Dar es Salaam, kwenye kongamano la vijana lililopewa jina la "Ushiriki wa vijana kwenye uongozi na mapinduzi ya nne ya viwanda".

Kongamano hilo lilihusisha vijana zaidi ya 100 kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Morogoro, Dodoma na Arusha.

"Someni na kutumia fursa zilizopo, lakini mkizingatia sana jinsi dunia inavyokwenda msije mkabaki nyuma wakati huu wa sayansi na teknolojia, kwani dunia sasa inakwenda kidigitali," alisema Prof. Ngowi.

Alisema, hata dunia ya viwanda inaendeshwa kidigitali na kuwataka wabadilike kuanzia shuleni hadi vyuoni hata katika kufanya biashara, kwa vile uchumi na kilimo kwa sasa vinaendeshwa kidigitali.

"Kwa sasa ni lazima kijana ujiulize kwanza kaam unakwenda kusoma, je unasoma nini? Bila kutambua hilo, fursa zinazojitokeza zinaweza kuwapita kwa sababu kuweka pembeni teknolojia," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), walioandaa kongamano hilo, Lilian Liundi, alisema matarajio yao ni kwamba kongamano hilo litakuwa sauti za vijana zinakazotoka na kusikika.

"Kwenye kongamano hili TGNP tunatumaini kuona vijana wanakuza uelewa wao, fursa na ushiriki wao kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda na ni malengo yetu kuhakikisha vijana na hasa wa kike hawaachwi nyuma," alisema.

Alisema, TGNP inatambua uchumi wa Tanzania umekuwa na taswira tofauti tangu uhuru mwaka 1961, tangu umiliki wa mkoloni, wa serikali kwenye ubinafsishaji na katika mabadiliko ya sera.

Sera ya maendeleo ya sasa imeleta tena maendeleo ya viwanda kwenye kipaumbele cha sera yetu na serikali imeongelea uchumi wa viwanda, lakini kidunia mapinduzi ya nne ya viwanda yamekuwa yakitekelezwa," alisema.

Alisema, vijana wanapoelewa fursa zinazoambatana nayo wataachwa nyuma na huenda wakajikuta wanabaki kulaumu serikali, na kwamba TGNP inatambua kuwa kila jambo linakuwa kidigitali.

"Hii inakuja na namna tofauti ya biashara, ya uongezaji wa thamani wa bidhaa zetu, mawasiliano na mengineyo yenye taswira ya kidigitali ikiwamo utafutaji wa masoko kwa bidhaa tunazoziandaa," alisema Liundi.

# Meli ya kisasa yajengwa kwa bil. 90/-

**Na Elizabeth Zaya,**
MWANZA

TANZANIA inajenga meli mpya ya kisasa ambayo itakuwa ya mfano katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Akizungumza na waandishi wa habari jijini Mwanza, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), Eric Hamissi, alisema Sh. bilioni 89.7 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa meli hiyo.

Alisema meli hiyo itajulikana kwa jina la MV Mwanza Hapa Kazi Tu. Alisema ujenzi wa meli hiyo umeanza na umefikia asilimia 50 na kwamba ujenzi wake utatumia miezi 24 kuanzia Januari mwaka huu hadi Januari mwaka 2021.

Hamissi alisema meli hiyo itakuwa na urefu wa mita 92.6, upana wa mita 17, kimo kwenda juu mita 11.2

Pia alisema itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 1200, magari 20 madogo, malori matatu na tani 400 za mizigo.

"Hakuna meli ya namna hii katika ukanda wote wa maziwa makuu, na ndiyo maana tunasema itakuwa ya mfano katika ukanda huu," alisema Hamissi.

Aliongeza: "Ujenzi wa meli hii ilikuwa ni ahadi iliyotolewa kujengwa nyingine baada ya kuzama ile meli ya Mv Bukoba, kwa hiyo tunashukuru ahadi hii imeanza kutekelezwa katika miaka minne ya serikali ya awamu ya tano."

Alisema meli hiyo inajengwa kwa kutumia fedha za ndani, na kwamba asilimia 40 ya fedha imelipwa kwa mkandarasi.

"Kazi ya kukata vyuma vya kutengeneza meli hii pamoja na 'material' mengine inafanyika Afrika Kusini, lakini vinaunganishiwa hapa kwetu," alisema Hamissi.

Alisema utengenezaji wa meli hiyo unafanywa na makandarasi watatu akiwamo Gas Entec, Kangnam Corporation wakishirikiana na SUMA JKT.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, akijumuika kucheza na mmoja ya wakazi wa mkoa huo, baada ya kuzindua kampeni maalum ya 'Haachwi Mtu Nyuma, Kamilisha Ujasili wako' ambayo imeandaliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa lengo la kuhamasisha wananchi kusajili upya laini zao za simu kabla ya mwisho wa mwezi. Kampeni hiyo ilizinduliwa Tabora mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Waomba DNA kuharakisha kesi

**Na Romana Mallya**

WAKATI vitendo vya ubakaji na ulawiti vikishamiri jijini Dar es Salaam, wadau wa sheria wameomba serikali iweke utaratibu wa waathirika wapimwe vina saba (DNA) ambavyo vitatoa ushahidi wa kutosha na kuharakisha kesi mahakamani.

Takwimu zinaonyesha katika kipindi cha miezi 10 mwaka jana matukio ya ubakaji yaliyoripotiwa Jeshi la Polisi jijini Dar es Salaam ni 608 na mwaka huu yameongezeka na kufikia 719 huku vitendo vya ulawiti vikiongezeka kutoka 259 mwaka jana na kufikia 319 mwaka huu.

Mkurugenzi wa Kituo cha Msaada wa Kisheria kwa Wanawake (WLAC), Wakili Theodosia Muhulo, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakiwa Shule ya Msingi Mburahati kwa ajili ya kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia.

Katika kampeni hiyo WLAC kupitia mradi wake ulioanza mwaka jana kwa shule 10 za jijini Dar es Salaam zilizokuwa na changamoto za matukio ya ukatili wa kijinsia ikiwamo ubakaji, ulawiti na unyanyasaji watoto, inaendelea kuwaelimisha wanafunzi namna ya kujilinda.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Wakili Muhulo alisema Januari hadi Novemba mwaka huu jumla ya kesi walizozipokea kituoni kwao ni 3,350 ambapo miongoni mwake zipo za ubakaji na ulawiti.

"Asilimia 90 ya kesi tulizopokea zinaukatili wa kijinsia kwenye masuala ya ndoa, kwa upande wa watoto zipo kesi za aina mbili zipo ambazo waliokinzana na sheria wenye makosa ya jinai kama kubaka watoto wenzao au kufanya unyanyasaji wa kingono," alisema.

Alisema katika kesi hizo zinazoongoza ni za ubakaji mtoto kwa mtoto au mtoto aliyefanyiwa na mtu mzima.

"Wengi ukiwahoji wanasema wamewahi kufanyiwa vitendo hivyo ndio maana na wao wanafanya, wengine wameshuhudia nyumbani wanakoishi na wengine wameona kupitia kwenye sinema zinazoonyeshwa mtaani," alisema.

Wakili Muhulo alisema kati ya kesi ambazo zimefika kituoni kwao baadhi tayari zimefika mahakamani lakini bado hazijafikia hatua ya hukumu.


"Changamoto ni upelelezi kuchukua muda mrefu hivyo kesi zinafika mahakamani na kuchukua na mwisho wa siku ushahidi unapotea na waathirika wanakosa haki.

"Ushahidi ni changamoto nyingine Tanzania, lakini kwa nchi nyingine mtu akisema amebakwa wanapima hadi DNA, sisi kwetu bado hatujafika hapo, hii inachangia kutopata ushahidi wa kutosha, mfano mtoto anafanyiwa tukio, lakini kudundulika ni baada ya miezi miwili."

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mburahati, Rejea Shemu, alitaja changamoto ambazo wanaziona kwa wanafunzi wake kuwa ni baada ya masomo wazazi au walezi kuwatumikisha kwenye shughuli za kiuchumi.

Alisema wamefanikiwa kupunguza changamoto hiyo ya vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto na kwa mwaka huu yametokea matukio mawili tu.

Mkaguzi Msaidizi Furaha Gunda kutoka kituo cha polisi Mburahati ambaye ni Mkuu wa Dawati la Kijinsia, alisema umaskini umekuwa ni changamoto kubwa inayosababisha wazazi badala ya kutafuta haki ya mtoto wao aliyebakwa au kulawitiwa, huamua kumalizana na mtuhumiwa kwa kuchukua fedha kidogo.



# Wanawake walia mfumo dume haki miliki ya ardhi

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WANAWAKE wa vijiji vinne vya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, wamekiri kuwa mila na desturi zinazokumbatiwa na wanaume zimekuwa kikwazo kwao kushindwa kuwa na haki ya kumiliki ardhi.

Walipaza sauti zao mwishoni mwa wiki wakati wakipewa mafunzo ya namna ya kupata haki ya kumiliki ardhi yaliyoandaliwa na Shirika lisilo la Kiserikali Cosita.

Wanawake waliohudhuria katika mafunzo hayo ya kuwajengea walitoka katika vijiji vya Kiongozi, Malangi, Chemchem na Mtuka.

Mwanaidi Ramadhan, mkazi wa kijiji cha Kiongozi akizungumza na Nipashe baada ya mafunzo hayo, alisema yatawabadilisha na watakwenda kutoa elimu kwenye jamii.

Alisema kwa kipindi kirefu wanaume wamewaonea wanawake, na kuwa baada ya kupata mafunzo hayo watakwenda kuleta mabadiliko katika jamii.

Philomena Homa kutoka kijiji cha Chemchem, alisema elimu waliyoipata itawasaidia kuamka na kudai haki yao ya kumiliki ardhi na mali katika jamii.

Homa alisema iwapo watapata ardhi itawasaidia kuinuka kiuchumi kwa kuwa wataitumia kufanya uzalishaji wa mali na hatimaye kuchangia shughuli za kimaendeleo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Cosita, Patrice Gwasma, alisema wanatekeleza mradi wa haki za ardhi kwa wanawake kwa unafadhiliwa na Shirika la Foundation for Civil Society (FCS).

Gwasma alifafanua kwa mujibu wa utafti wa kamisheni ya umoja wa mataifa uliofanyika mwaka 2012, kwa kishirikiana na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden (SIDA), lililofanya utafiti mwaka 2015 na kubaini asilimia 20 ya wanawake duniani ndio wanamiliki ardhi.

Alisema asilimia 80 ya wanawake duniani hawamiliki ardhi, hivyo ameitaka jamii kubadilika na kutoa elimu ili wanawake na wanaume wote wawe na haki sawa ya umiliki ardhi.

Naye Mratibu wa Mradi wa Haki za Ardhi kwa Wanawake, Paulo John, akizungumza na wanawake hao, alisema vyanzo vya migogoro ni watu kutokufahamu sheria za ardhi.

Alisema mwanamke ana haki ya kumiliki ardhi kwa mujibu wa sheria namba 4 na namba 5 ya mwaka 1999, kifungu cha 3(2) ambacho kinampa haki mwanamke ya kumiliki, kutumia na kuuza au kuigawa ardhi sawa na haki aliyonayo mwanaume.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo (katikati), akikata utepe ishara ya kupokea gari aina ya V8 iliyotolewa na wadau wa usalama barabarani kwa ajili ya kutumiwa na Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa wa Arusha. **PICHA: WAOINDE SHIZZA**

# Serikali yapoteza bil. 5/- biashara magendo mifugo

**Na Daniel Sabuni,** LONGIDO

SERIKALI imekuwa ikipoteza mapato kati ya Sh. bilioni nne hadi tano kwa mwaka, kutokana na uuzwaji wa mbuzi kwa magendo kwenda Kenya.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema serikali imekuwa ikikosa mapato hayo kwa kipindi cha miaka mingi kutokana na mifugo hiyo, kwenda kuuzwa Kenya kupitia mpaka wa Namanga.

Hata hivyo, alisema serikali hadi kufikia mwaka jana, imefanikiwa kudhibiti uuzwaji wa mifugo nje ya nchi ili kuokoa fedha zilizokuwa zinapotea.

"Mbuzi walikuwa wakiuzwa kwa njia za magendo na njia halali, lakini njia ya magendo ilikuwa ikiuza mbuzi wengi zaidi... tumechukua hatua kama kudhibiti na tumekuwa wakali sana, na tumeshaeleweka sasa mambo yanakwenda vizuri," alisema Mwaisumbe.

Alisema ilibidi serikali kuwa wakali ili kurudisha hali ya uhalali wa biashara ya mbuzi, na wakati mwingine walikuwa wakitaifisha mifugo iliyokamatwa kutoka kwa wafanyabiashara walioukuwa wakiuzwa kwa njia za magendo.

"Tukikamata mbuzi na kugundua wanauzwa kwa magendo tunataifisha, maana siwezi kuona serikali inakosa mapato kutokana na tamaa za watu wachache, suala hili niko makini... naomba wafanyabiashara wanielewe, mapato ndio yanamsaidia Rais John Magufuli katika juhudi zake za kueleKeza Watanzania kwenye uchumi wa kati na kupunguza umaskini," alisema Mwaisumbe.

Aidha, alisema ameshawezesha wafanyabiashara hao kuunda vikundi vya watu kati ya 30 hadi 45 na kuvirasimisha ili kukaa pamoja na kuangalia mianya ya upotevu wa mapato ya serikali sambamba na kufanya tathmini ya mafanikio ya wafanyabiashara.

Alisema vikundi hivyo vitawasaidia kuwa na umoja ambao utaunganisha nguvu za pamoja na hata kusafirisha kwa pamoja mbuzi hao, kwa njia halali ili nchi ipate kodi kwa ajili ya maendeleo ya watu wake.

"Tumedhibiti kwa asilimia 90 uuzwaji holela wa mbuzi wa magendo, lakini kwa ushirikiano wa pamoja, wafanyabiashara matarajio yetu ni kufikia asilimia 100," aliongeza Mwaisumbe.

Alisema hivi karibuni, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, atafika wilayani humo kwa ajili ya kuangalia masuala ya mifugo pamoja na maboresho mbalimbali yanayohitajika.

# Madalali madini bila leseni wapigwa 'stop'

**Na Allan Isack,** MIRERANI

MADALALI na wafanyabiashara wa madini ya Tanzanite Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wasiokuwa na leseni ya biashara ya madini wamepigwa marufuku ya kujihusisha na shughuli hiyo.

Ofisa Madini Mkazi wa Mirerani, Daudi Ntalima, alisema juzi kuwa dalali au mfanyabiashara asiyekuwa na leseni ya biashara ya madini, haruhusiwi kujihusisha na biashara hiyo.

Ntalima alisema pia wafanyabiashara wa madini wasiokuwa na leseni hawaruhusiwi kufika kwenye chumba cha uthaminishaji kwa ajili ya kuhifadhi au kuthaminisha madini.

Alisema wenye leseni za biashara ya madini hawatakiwi kutumiwa na watu wasiokuwa na leseni za madini kwa ajili ya kuwatolea madini nje ya ukuta wa Mirerani.

Alisema wenye leseni ya biashara ya madini ya Tanzanite wanakumbushwa kuendelea kuwasilisha taarifa za ununuaji na mauzo ya madini yao.

"Wamiliki wa leseni za biashara ya madini mnapaswa kuwa na chombo maalumu cha kuhifadhi madini yenu ndani ya getini mkiwa mmefunga kwa kufuli maalumu," alisema Ntalima.

Aliwataka wamiliki wa leseni za biashara ya madini kukamilisha malipo ya tathmini ya madini husika uliofanyiwa uthaminishaji kama ilivyoandikwa katika hati ya madai.

Alisema wahusika wote wanapaswa kutekeleza maelekezo hayo, kwa kuwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa atakayekiuka agizo hilo.

Mmoja wa madalali wa eneo hilo, Cosmas John, alisema wadau wa madini wanapaswa kubadilika na kutii maagizo ya serikali kwa kuwa mfumo wa sasa umebadilika tofauti na miaka ya nyuma.

Kwa upande wake Samwel Mollel, alisema bado madalali wanapambana kukata leseni ya madini ili wawe na fursa ya kufanya biashara hiyo kwa kutambuliwa.

## Kuchelewa kituo kwamchefua DC

**Na Mwandishi Wetu,** ROMBO

KUCHELEWA kutekelezwa kwa mchakato wa uanzishwaji wa kituo jumuishi cha pamoja kinachosaidia kufuatilia kwa karibu huduma za uchunguzi na tiba kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia, kumemsikitisha Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo.

Kutokana na kusuasua kwa utekelezaji wake, Hokororo ameitaka Idara ya Maendeleo ya Jamii ya Halmashauri ya Wilaya hiyo kuanzisha mara moja kituo hicho kitakachotoa huduma hiyo ili kupa nguvu mkakati wa serikali wa kukabiliana na matukio ya ukatili.

Alikuwa akizungumza mwishoni mwa wiki na wakazi wa Tarakea walioungana na Jukwaa la Vuguvugu la Ukombozi wa Mwanamke Kimapinduzi (Tapo), kuadhimisha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia. Maadhimisho hayo hufanyika kuanzia Novemba 25 hadi Desemba 10 kila mwaka.

"Nimewasikia wananchi niliowapokea hapa Kata ya Nanjara, Tarakea wakati wa maandamano yenu mkiomba serikali isimamie haraka suala la uanzishwaji wa One Stop Centre (Kituo Jumuishi cha Pamoja), mimi nashanga ni kwa nini hadi leo hakijaanzishwa wakati ni agizo la serikali.

Hokororo alisisitiza: "Nawakumbusha tena watu wa maendeleo ya jamii kuacha kigugumizi katika kukianzisha, ni muhimu sana kikawepo katika Wilaya ya Rombo, na hili ni jambo ambalo linaupa nguvu pia Mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (Mtakuwa) kuonyesha matokeo chanya."

Kituo jumuishi cha pamoja kinahusisha matabibu, maofisa wa dawati la jinsia la Polisi, maofisa maendeleo ya jamii, ustawi wa jamii na wadau wanaoshughulikia mashauri ya ukatili wa kijinsia.

Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Rombo, Regina Futakamba, akitoa mada kuhusu matendo ya ukatili wa kijinsia na miongozo ya sheria, alisema kesi nyingi zinazofikishwa katika mahakama hiyo kwa sasa zinahusu zaidi matukio ya ubakaji wa watoto wenye umri chini ya miaka 12.

"Hakuna mtoto aliyefika mahakamani kutoa ushahidi akawa amebakwa mara moja, wote wanaoletwa wameingiliwa zaidi ya mara moja. Sasa madaktari wanaokuja kutoa ushahidi baada ya kuwafanyia vipimo watoto hao wanaodaiwa kubakwa, huthibitisha kwamba watoto hao huwa wamebakwa zaidi ya mara moja.

Hakimu Futakamba aliongeza: "Kina mama kabla ya kujitokeza kupinga ukatili huu, turudi kwanza katika jukumu letu la msingi la malezi bora, tufuatilie watoto wetu. Tumejikita zaidi katika kutafunga pesa (fedha) badala ya kuhudumia familia. Kilimanjaro nimeona karibu kila mwanamke anachakarika kwenye biashara kuanzia tarehe moja hadi mwisho wa mwezi, hii haifai."

# Msekwa aahidi MoCU kuzalisha wasomi mahiri

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SPIKA wa zamani wa Bunge la Tanzania, Pius Msekwa, amesema chini ya uongozi wake kama Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), atahakikisha anasimamia jukumu la msingi la chuo hicho kuzalisha wasomi mahiri wa fani za ushirika na biashara ambao hawatatiliwa mashaka katika weledi wao.

Msekwa aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati akiwatunuku astashahada, stashahada, shahada ya kwanza na shahada ya uzamili, wasomi 1,773 wa chuo hicho.

Alisema kati ya wahitimu hao, wamo nguli wa kitaaluma walioandaliwa kulisaidia taifa kuja na matokeo chanya ya tafiti mbalimbali zinazohusu maendeleo ya ushirika na biashara nchini.

Kwa mujibu wa Msekwa, kundi hilo la wasomi linaloingia katika soko la ajira ni mahusus kwa ajili ya kujenga uchumi na kupunguza umasikini, wakati Tanzania ikijielekeza kuufikia uchumi wa kati wa viwanda ifikapo mwaka 2025. "Chuo hiki ni miongoni mwa vyuo vikuu vya umma vilivyo chini ya Wizara ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, tumepewa jukumu zito la kuandaa wataalamu wa fani mbalimbali wakati huu taifa likielekea katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

"Katika kipindi cha mwaka wa masomo 2018/2019 tumefanikiwa kulisaidia taifa kuzalisha wataalamu hao 1,773. Tujipange zaidi kutekeleza majukumu yetu kama kutoa huduma za ushauri unaohusiana na maendeleo ya ushirika na biashara kwa wadau wa ushirika, asasi za biashara na watu binafsi."

Wanataaluma hao wanatoka katika Kitivo cha Ushirika na Maendeleo ya Jamii (FCCD), Kitivo cha Biashara na Sayansi za Mawasiliano (FBIS), Kurugenzi ya Maktaba ya Ushirika na Nyaraka za Kale (DLS) na Taasisi ya Elimu Endelevu ya Ushirika (ICCE).

Awali, Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Alfred Sife, alisema kati ya wanataaluma hao waliohitimu mafunzo ya muda mrefu, limo kundi la wahitimu katika programu za Shahada ya Umahiri ya Ushirika na Maendeleo ya Jamii (MACCD), Shahada ya Umahiri ya Menejimenti ya Manunuzi na Ugavi (BA-PSM) na Shahada ya Umahiri ya Menejimenti ya Biashara (MBM).

Oktoba 21 mwaka huu, Msekwa alimthibitisha rasmi Prof. Alfred Said Sife kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), baada ya kuwabwaga maprofesa wengine saba katika kinyang'anyiro cha kumsaka makamu mkuu wa chuo hicho.



Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Alvera Ndabagoye, akijibu maswali yaliyoulizwa na madiwani wa halmashauri hiyo, katika kikao cha madiwani wakati wa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya kwanza ya Julai -Septemba 2019. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Mageuzi makubwa miundombinu Hai

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

SERIKALI imepanga kuja kufanya mageuzi makubwa ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai, baada ya kuthibitisha itaanza rasmi kuzijenga kwa kiwango cha lami nyepesi barabara zake za Mji wa Mdogo wa Bomang'ombe.

Jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Yohana Sintoo, alithibitisha kuwapo kwa mpango huo kuanzia mwaka ujao.

"Ni kweli halmashauri ninayoingoza kama mtendaji mkuu, ina nia ya dhati ya kuzijenga kwa kiwango cha lami barabara zote za mji wa Bomang'ombe. Hatua hii ina lengo la kuondoa kero ya ubovu wa miundombinu na kupendezesha mandhari ya mji," alieleza Sintoo.

Alisema uamuzi huo utaufanya mji wa Bomang'ombe usionekane tena kama kijiji kutokana na barabara zake kukosa lami na nyingine kuwa na mashimo mengi ambayo yamekuwa yakisababisha ajali.

Aidha, Mkurugenzi huyo alisema ujenzi wa barabara hizo utakuwa unatekelezwa kwa awamu na pia zitajengwa kwa kiwango kinachotakiwa.

Wiki iliyopita, Baraza la Madiwani la Wilaya hiyo likiongozwa na Mwenyekiti wake, Helga Mchomvu lilikubaliana na wazo la Sintoo la kutaka kufanyika mageuzi katika sekta ya barabara, wakiazimia kuanza kwa utekelezaji wake mwaka ujao.

Pamoja na mambo mengine, utaratibu mpya ulioanzishwa na Mkurugenzi huyo wa kuwabana watumishi wa umma kila Jumatatu kuwasilisha ripoti ya namna wanavyowajibika kuhudumia wananchi, umepokelewa kwa shangwe na baadhi ya wakazi wa mji wa Bomang'ombe.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana kuhusiana na mkakati huo wa Sintoo kujiimarisha kiutendaji, baadhi ya wananchi hao Benedict Swai na Anjela Erick ambao ni wakazi wa Gezaulole, wilayani hapa walisema sasa ni dhahiri kwamba ule urasimu uliokuwa ukifanywa na baadhi ya watumishi wa umma umepata dawa.

Swai aliongeza: "Heshima imerudi, nilipata taarifa huyo Mkurugenzi aliwaambia kuwa hizi kazi tunatakiwa kuzifanya kwa kuheshimiana wakati wa kutekeleza majukumu yao, kwa sababu hao wananchi, ndio Mheshimiwa Rais Dk. John Magufuli amekuwa anasisitiza kila mara, ndio watu muhimu wanaotakiwa kutangulizwa mbele kuhudumiwa."

# NYOTA WALIOJIWEKA SOKONI DIRISHA DOGO



Mshambuliaji wa Polisi Tanzania, Ditram Nchimbi (kushoto), akiwania mpira na Lamine Moro kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Yanga ambayo alipiga hat-trick wakati zikitoka sare ya mabao 3-3.

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha dogo la usajili Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi Daraja la Kwanza likitarajiwa kufunguliwa Desemba 15 hadi Januari 15 mwakani, kuna baadhi ya wachezaji ambao kutokana na viwango vyao wamejiweka kwenye soko.

**Pamoja na Ligi Kuu kufikia raundi ya 13 tu, baadhi ya wachezaji hasa wa Kitanzania wanaocheza kwenye timu mbalimbali za mikoani na hata jijini Dar es Salaam wameonekana kuwa na uwezo mkubwa kiasi cha kuzuka wasiwasi kuwa huenda hawatoweza kuzichezea tena timu zao na kuchukuliwa na timu kubwa zenye uwezo wa kifedha.**

Msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara umekuwa mgumu kutokana na timu nyingi kujizatiti, lakini kikubwa na uwezo mkubwa unaoonyeshwa na wachezaji wengi na timu zinazoitwa au kujiita ndogo.

Timu za Simba, Yanga na Azam mpaka sasa ndizo hapa nchini zinazoonekana si tu kuwa na uchumi, lakini zina uwezo wa kumchukua mchezaji yeyote kutoka kwenye klabu yoyote ile.

Na zinavyoonekana zina mapungufu mengi, hivyo wala haipingiki kuwa zinaingia kwenye kinyang'anyiro cha kusaka wachezaji wa kuongeza nguvu kwenye timu zao.

Tayari baadhi ya wachezaji wameshaanza kuhusishwa na timu hizo. Mwandishi wa makala haya amekusanya majina ya wachezaji ambao wameonyesha viwango vya hali ya juu kwenye timu wanazochezea na kujiweka sokoni kwa klabu kubwa, hivyo huenda nusu msimu ujao wasiwe na klabu wanazochezea kwa sasa, hawa hapa...

**1. DITRIM NCHIMBI- POLISI TANZANIA**

Ni straika aliyeibuka ghafla na kuwa mmoja wa wachezaji tishio kwenye Ligi Kuu ya Tanzania. Hat-trick aliyoipiga kwenye mechi ambayo timu yake ilicheza dhidi ya Yanga na kutoka sare ya mabao 3-3, ilimfanya aitwe kwenye kikosi cha Taifa Stars na huko ameendelea kufanya vizuri pia.

Nchimbi anaichezea Polisi Tanzania kwa mkopo akitokea Azam FC. Ana misimu takriban mitano kwenye ligi akizichezea klabu za Njombe Mji, Majimaji, Mbeya City, Mwadui na baadaye Azam FC ambayo ilimtoa kwa mkopo Polisi Tanzania. Ana mabao manne mpaka sasa. Huenda Azam FC ikamrejesha nyumbani kwenye kipindi cha dirisha dogo kutokana na kiwango kikubwa alichokionyesha.

**2. BAKARI MWAMNYETO- COASTAL UNION**

Ni beki wa Coastal Union na timu ya Taifa, Taifa Stars. Kwa muda mfupi tu ametokea kuwa mahiri na maarufu kwa mashabiki wa soka nchini hasa anaposimama kati akiwa na mabeki mahiri, Kelvin Yondani, au Erasto Nyoni kwenye kikosi cha timu ya taifa.

Kutokana na kiwango chake cha sasa tayari klabu za Simba na Yanga zinaonekana kumnyemelea kipindi cha dirisha dogo. Huenda nusu msimu ujao asiichezee tena Coastal Union.

**3. AWESU AWESU- KAGERA SUGAR**

Kama unakumbuka misimu mitatu iliyopita, mchezaji huyo aliichezea Madini FC ya Arusha na kuwa mwiba mkali kwa Simba, timu hizo zilipocheza michuano ya FA Cup. Ilibaki kidogo Simba imsajili, lakini haijulikani nini kilitokea.

Kiungo huyo aliibukia Mwadui na kuichezea kwa misimu miwili na sasa yupo Kagera Sugar akiwa kwenye kiwango cha hali ya juu. Ni kiungo kwenye ufundi mwingi, pasi safi za mwisho, pia akiwa na uwezo wa kufunga. Amefunga mabao manne mpaka sasa. Wala haitoshangaza kumuona akiondoka Kagera Sugar kipindi cha dirisha dogo.

**4. DARUWESHI SALIBOKO- LIPULI FC**

Ni kiungo ambaye kwa sasa yuko kwenye kiwango cha hali ya juu. Saliboko ana mabao manne mpaka sasa, lakini akiwa amefunga hat-trick aliyoipata kwenye mechi ambayo Lipuli iliikanyaga Singida United mabao 5-1. Mchezaji huyu anahusishwa kujiunga na Yanga, hivyo haitoshangaza kama akiondoka Lipuli dirisha dogo.

**5. ADAM ADAM- JKT TANZANIA**

Tangu msimu uliopita akiwa na klabu ya Prisons alionyesha uwezo mkubwa wa kufunga mabao.

Ilionekana kama vile anabahatisha. Msimu huu akiwa na klabu mpya ya JKT Tanzania ameshapachika mabao manne mpaka sasa. Ni mmoja kati ya mastraika wanaochipukia kwa kasi.

Kwa uwezo alionao wala haitoshangaza kuona klabu kubwa zikipigana vikumbo kutafuta saini yake kipindi cha dirisha dogo.

**6. PAUL NONGA- LIPULI FC**

Ni straika mkongwe aliyechezea klabu mbalimbali nchini ikiwamo Yanga. Kwa sasa yupo Lipuli kwa misimu miwili na amekuwa akifanya vizuri, akiwa na mabao sita mpaka sasa.

Amekuwa akihusishwa kujiunga Simba, Azam au Yanga, ingawa mwenyewe amebainisha kuwa hatojiunga na Yanga kwa sababu alishawahi kucheza na mambo aliyokutana nayo huko hatamani kurejea.

**7. PETER MAPUNDA- MBEYA CITY**

Kama kuna mchezaji rahisi wa kumnasa dirisha dogo basi atakuwa ni Peter Mapunda. Kwa sababau pamoja na uwezo wake mkubwa anaouonyesha uwanjani, lakini timu yake haifanyi vema na inaonekana inakatisha tamaa.

Mapunda mwenye mabao matano, ni mtaalamu wa kupiga penalti na faulo. Mabao yake mengi ameyafunga kwa staili hiyo, lakini pia akiwa mahiri kucheza winga ya kushoto na kulia.

**8. GERALD MATHIAS- MWADUI FC**

Kama itakumbukwa, straika huyu ndiye aliyetia mchanga kwenye kitumbua cha Simba na kuwafanya viongozi kumtazama kwa jicho la tatu kocha Patrick Aussems kabla ya kumtimua. Alifunga bao pekee Mwadui ikiichapa Simba bao 1-0 na kutibua rekodi yake.

Ameshafunga mabao manne mpaka sasa, huku akihusishwa kwenda Yanga kwenye kipindi cha dirisha dogo.

**9. SAMSON MBANGULA- PRISONS**

Ni mmoja wa viungo wa kati wanaoing'arisha Prisons kwa sasa kiasi cha kuweka rekodi ya kutofungwa mechi yoyote mpaka sasa. Mbangula alivutia umati kwenye mechi dhidi ya Simba Uwanja wa Uhuru alipowafunika viungo wa Simba, mechi ambayo timu hizo zilitoka sare ya bila kufungana. Inasemekana viongozi wa Yanga wameonyesha nia ya kusajili.

**10. INNOCENT EDWIN- BIASHARA**

Ni straika ambaye ana mabao matatu mpaka sasa. Kwa timu anayochezea na uwezo wake huenda akanyakuliwa na timu yoyote ile hata KMC kwenye kipindi cha dirisha dogo.

**NJE YA UWANJA**

JOSE Mourinho ameshuhudia kikosi chake cha Tottenham kikifunga mabao matano (5-0) dhidi ya Burnley kwenye Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza tangu Januari 2015, wakati akiiongoza Chelsea kushinda 5-0 dhidi ya Swansea. Kipindi akiinoa Manchester United haikuwahi kufunga zaidi ya mabao manne kwenye mechi 93 alizoiongoza klabu hiyo.





# NYOTA WA5 WALIOCHEMKA EPL WAKANG'ARA KWINGINE

**LONDON,** England

LIGI Kuu ya England inachukuliwa kuwa moja ya ligi yenye ushindani mkubwa zaidi na mashabiki wengi wa soka dunini, lakini licha ya hilo si wachezaji wote bora duniani wamepata mafanikio pale.

**Wachezaji wakubwa kama Cristiano Ronaldo, Thierry Henry na Sergio Aguero wote wamecheza kwenye ligi hiyo na wamekuwa magwiji wakati wao wa uchezaji, lakini wachezaji wengine wameshindwa kupata mafanikio licha ya kung'ara sehemu nyingine.**

Kwa sababu mbalimbali, staili ya maisha imekuwa ni tatizo kuweza kuzoea soka la Uingereza na hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao walishindwa kung'ara kwenye Ligi Kuu ya England, lakini wakapata mafanikio sehemu nyingine duniani.

### 1. MEMPHIS DEPAY

Mshambuliaji huyu wa Uholanzi, Memphis Depay alijiunga na Manchester United akitokea PSV Eindhoven kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2015 kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 25, na mchezaji huyo ambaye alikuwa na umri wa miaka 21, alikwenda pale Old Trafford akiwa na matumaini makubwa.

Alifunga mabao 22 katika mechi 30 alizocheza kwenye Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, akiwa na PSV na baadhi ya mashabiki walimlinganisha na Cristiano Ronaldo na Arjen Robben.

Pale United Mholanzi huyu alikumbana na wakati mgumu. Kwani licha ya kuanza kucheza mechi 29 za Ligi Kuu katika msimu wake wa kwanza, Memphis alifunga mabao mawili tu, na mara nyingi akajikuta akikaa benchi kutokana na kiwango chake kushuka.

Mwanzo wa msimu wa 2016/17, ulikuwa mbaya zaidi kwake, alicheza mechi nane tu kwa 'Mashetani Wekundu' hao katika mashindano yote kabla ya kuuzwa kwa klabu ya Ufaransa, Lyon Januari 2017 kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 16.

Akiwa Lyon tayari amefunga mabao 50 katika mechi 130 yakimwamo mabao 11 katika mechi 14 msimu huu na amejiimarisha mwenyewe kwenye kikosi cha kwanza cha timu ya Taifa ya Uholanzi.

### 2. FLORIAN THAUVIN

Winga wa Ufaransa, Florian Thauvin alisajiliwa Newcastle United akitokea Marseille kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2015 kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 15. Thauvin alikuwa akitambulika kama mmoja wa wachezaji bora barani Ulaya, na alitajwa kuwa mchezaji bora kijana wa mwaka wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, msimu wa 2012/13.

Bahati mbaya pale kwenye dimba la St. James' Park mambo yalikuwa magumu kwa upande wake; alicheza mechi 16 kwa klabu hiyo, akifunga bao moja kwenye mchezo wa EFL dhidi ya Northampton Town, na alishutumiwa hata na gwiji wa klabu hiyo, Alan Shearer. Hakukuwa na mshangao kwa Mfaransa huyo alipopelekwa kwa mkopo pale Marseille ikiwa ni miezi mitano baada ya kutua England.

Thauvin alihamia moja kwa moja kipindi cha majira ya joto mwaka 2016 na tangu hapo amekuwa kwenye kiwango kikubwa zaidi tofauti na alivyokuwa akicheza kule Ligi Kuu ya England. Winga huyo amefunga mabao 15 kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, katika msimu wa 2016/17 ikiwamo 'hat-trick' yake ya kwanza na msimu uliofuata alifunga mabao 22 katika mechi 34. Na hilo likatosha kumfanya kuwa mchezaji bora wa mwaka wa Ligi Kuu ya Ufaransa na pia alikuwa kwenye kikosi kilichotwaa Kombe la Dunia mwaka 2018.

### 3. GERARD PIQUE

Haifai kumuita Gerard Pique kwamba alishindwa kung'ara pale Manchester United, lakini beki huyo wa kati wa Hispania alitumia misimu minne akiwa pale Old Trafford ingawa haikuwa mizuri kwake. Akiwa na umri wa miaka 20, msimu wa 2007/08, ukamfanya kocha gwiji wa United, Sir Alex Ferguson kumuona hafai.

Halikua jambo la kushangaza wakati alipouzwa kwenda Barcelona klabu ya utotoni mwake kipindi cha majira ya joto mwaka 2008. Na tangu hapo amekuwa na mafanikio makubwa zaidi kwa klabu hiyo ya Nou Camp.

### 4. RADAMEL FALCAO

Kwa kipindi cha muongo mmoja uliopita, Radamel Falcao wa Colombia amekuwa mmoja wa washambuliaji bora duniani. Amefunga mabao mengi akiwa nchini Ureno, Hispania na Ufaransa na kwa sasa anacheza nchini Uturuki.

Lakini kwa bahati mbaya, Falcao ambaye anajulikana kwa jina la utani la 'El Tigre' alishindwa kung'ara kule kwenye Ligi Kuu ya England.

Falcao alichipukia akiwa Porto baada ya kujiunga nao msimu wa 2008/09, na alifunga jumla ya mabao 34 katika mechi 43 alizocheza kwenye mashindano yote kabla ya kufunga mabao 38 katika mechi 44 msimu uliofuata.

Usajili wake wa kutua pale Atletico Madrid ulifuata na Falcao aliweza kujiimarisha yeye mwenyewe kwa kushinda Kombe la Ligi ya Europa mwaka 2012 na akifunga mabao 70 katika mechi 91 alizoichezea klabu hiyo kwa kipindi cha misimu miwili. Kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2013 alisajiliwa Monaco.

Halafu baadaye akapelekwa kwa mkopo Manchester United na kwa bahati mbaya hakuweza kabisa kuwa na mafanikio kwenye Ligi Kuu ya England. Akiwa pale Old Trafford alifunga mabao manne tu. Baadaye akapelekwa kwa mkopo Chelsea - ambako alicheza mechi 12 na kufunga bao moja.

Falcao alirudi tena Monaco baada ya kushindwa kutamba pale Chelsea na kwa msimu wa 2016/17 - tayari amefunga mabao 30 katika mechi 43.

### 5. PAULINHO

Alisajiliwa Tottenham Hotspur kipindi cha majira ya joto mwaka 2013 wakati Andre Villas-Boas akijaribu kukijenga kikosi chake baada ya kuuzwa kwa Gareth Bale kwenda Real Madrid kwa pauni milioni 80.

Paulinho raia wa Brazil aliigharimu Spurs ada ya pauni milioni 17, lakini kwa bahati mbaya alijikuta kwenye wakati mgumu pale.

Aliuzwa kwenda Ligi Kuu ya China katika klabu ya Guangzhou Evergrande na kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2017, aliuzwa Barcelona na alicheza kwa mwaka mmoja tu kabla ya kurudi China, ambako alifunga mabao tisa katika mechi 49.



Gerard Pique na mkewe Shakira.

## Nukuu

"Mbio za ubingwa zimeshaisha. Kwa kile ninachokisoma, hakuna mtu anayetupa sisi nafasi. Imeshamalizika. Kwa mfano tuna mchezo dhidi ya Liverpool, itakuwa ni uchizi kufikiria kuhusu ubingwa, kwa uhakika kabisa," **Pep Guardiola kabla ya Man City kuiangukia pua dhidi ya Man United juzi.**



"Uamuzi umefanywa na waandishi wa habari, sahihi? Ninaona ni tofauti kidogo. Lionel Messi labda ni mchezaji bora niliyewahi kumuona katika maisha yangu, ila msimu uliopita kamwe siwezi kukumbuka zaidi msimu wa kuvutia kwa beki. Ingekuwa sahihi kama Virgil angeshinda pia 'Ballon d'Or'. Tulishinda Ligi ya Mabingwa na alikuwa na msimu mzuri," **Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp**



"Rekodi zinawekwa ili zivunjwe, lakini sijui ni nani na lini. Lakini kwa wakati huu naishikilia rekodi hii [kutwaa 'Ballon d'Or' mara sita] na nina furaha kubwa. Ilikuwa ni jambo lisililofikirika kushinda moja na baadaye sita," **Lionel Messi baada ya kuweka rekodi ya kutwaa Ballon d'Or mara sita wiki iliyopita.**





# USIYOYAJUA CHALLENGE CUP IKIENDELEA UGANDA

Kikosi cha Zanzibar Heroes kilichofika fainali ya Kombe la Chalenji 2017 nchini Kenya na kufungwa na wenyeji kwa mikwaju ya penalti 3-2, baada ya kufungana mabao 2-2 kwa dakika 120.

**Na Adam Fungamwango**

MICHUANO ya Kombe la Chalenji wanaume Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), imeanza kutimua vumbi tangu juzi, Jumamosi nchini Uganda, ikizishirikisha jumla ya timu tisa, zikigawanyika makundi mawili A na B.

**Kundi A, linazishirikisha timu za Burundi, Djibouti, Eritrea, Somalia na Uganda, huku Kundi B likiwa na timu za Tanzania Bara maarufu kama Kilimanjaro Stars, Kenya, Sudan na Zanzibar (Zanzibar Heroes).**

Awali kulikuwa na makundi matatu, lakini kutokana na kujitoa kwa timu nne, Shirikisho la Vyama vya Soka Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati(Cecafa) ikapunguza makundi, ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya ratiba yenyewe.

Jumamosi iliyopita, Djibouti ilitoka sare ya bila kufungana dhidi ya Somalia na Uganda ikiichapa Burundi mabao 2-1.

Sare ya Djibouti dhidi ya Somalia inaweka rekodi ya timu hizo kukutana mara nane, huku mara nne ikiwa ni kwenye michuano hiyo.

Kwenye mechi nane ambazo zimecheza, Somalia imeifunga Djibouti mara tatu, sare tatu, huku ikifungwa mara mbili. Kwenye michuano hiyo ya Cecafa, kila timu imeshinda mara moja kila mmoja akishinda mabao 2-1 na sare mbili ambazo zote ni za bila kufungana.

Jana kulikuwa na mechi nyingine, Kilimanjaro Stars ikicheza dhidi ya Mabingwa Watetezi Kenya na Zanzibar ikacheza na Sudan.

Mwandishi wa makala haya amekusanya rekodi, takwimu na dondoo mbalimbali za michuano hiyo inayoendelea kufanyika nchini Uganda, hizi hapa...

### 1. KUTOKA GOSSAGE MPAKA CHALLENGE CUP

Michuano hii zamani iliitwa Gossage Cup na ilianzishwa mwaka 1926 enzi za mkoloni hadi mwaka 1966 ilipobadilishwa na kuwa Challenge Cup kuanzia mwaka 1967.

Ilijulikana kama Gossage Cup kutokana na kudhaminiwa na Kampuni ya Sabuni chini ya mmiliki William Gossage.

### 2. KENYA YA KWANZA KUTWAA KOMBE

Timu ya Taifa ya Kenya, Harambee Stars ambao ni mabingwa watetezi ndiyo timu ya kwanza kutwaa kombe hilo, wakati linaitwa Gossage na pia wakati lilipobadilishwa na kuitwa Challenge Cup.

Mwaka 1926, ilipofanyika kwa mara ya kwanza ikiitwa Gossage iliichapa Uganda mabao 2-1 na mwaka 1967, ilipobadilishwa na kuitwa Challenge Cup ilitwaa kombe hilo ambalo lilichezwa kwa mtindo wa ligi kwa kushinda mechi zote tatu kwa kuzifunga timu za Uganda mabao 3-1, Zanzibar mabao 6-0 na Tanzania Bara mabao 5-3, hivyo kufikisha pointi sita. Ikumbukwe wakati huo timu ikishinda inapata pointi mbili tu na si tatu kama hivi sasa.

### 3. UGANDA MABINGWA WA KIHISTORIA

Timu ya Taifa ya Uganda, maarufu Uganda Cranes ndiyo timu iliyotwaa mara nyingi zaidi kuliko timu nyingine.

Timu hiyo imechukua mara 14, ikifuatiwa na Kenya ambayo imetwaa mara saba, Tanzania Bara, Zambia na Malawi zimechukua mara tatu kila moja, Sudan mara mbili, huku, Rwanda Zimbabwe na Zanzibar zikichukua mara moja. Hii haijumlishi wakati ikiitwa Gossage.

Lakini hata ukijulisha na wakati wa Gossage kuanzia mwaka 1926, bado Uganda wanabaki vinara kwani wanakuwa wamechukua mara 39, Kenya mara 21, Tanzania Bara mara nane, Ethiopia mara nne, Malawi na Zambia mara tatu, Sudan mara mbili, Rwanda Zimbabwe na Zanzibar mara moja.


### 4. ZANZIBAR FAINALI MSIMU ULIOPITA

Ikumbukwe kuwa michuano hiyo haikuchezwa mwaka jana 2018, lakini mara ya mwisho 2017, Zanzibar ambayo inachukuliwa poa ilitinga hatua ya fainali na kuwachachafya wenyeji Kenya kwa kutoka sare ya mabao 2-2, kabla ya kufungwa kwa mikwaju ya penalti 3-2.

### 5. KILI STARS KUCHAPWA NA ZANZIBAR

Wakati kesho Jumanne Kilimanjaro Stars ikitarajiwa kucheza dhidi ya ndugu zao, Zanzibar Heroes, rekodi inaonyesha kuwa mara ya mwisho zilipokutana kwenye michuano hiyo mwaka 2017, Tanzania Bara ilichapwa mabao 2-1 nchini Kenya, mechi ikichezwa Uwanja wa Machakos, mabao yakizamishwa nyavuni na Kassim Selemani Selembe na Ibrahim Hamadi Hilika, huku la Bara likifungwa na Mao Mkami.

**NAJUA WAJUA**



MLINDA mlango wa Barcelona, Marc-Andre ter Stegen ni kipa pekee kwenye ligi tano bora barani Ulaya msimu huu kuweza kutoa pasi mbili za mwisho [assist].

## SOKA



# WACHEZAJI WA5 WAKUTAZAMWA UEFA

**PARIS,** Ufaransa

BAADA ya kusimama kwa wiki moja, Ligi ya Mabingwa Ulaya inarudi tena wiki hii. Wachezaji wengi wamekuwa waking'ara kwenye mashindano hayo makubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Ulaya.

**Makala haya yanakuchambulia wachezaji watano wa kutazamwa zaidi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu...**

### 5. SERGE GNABRY

Serge Gnabry ni moja ya bidhaa adimu barani Ulaya kwa sasa. Arsenal watakuwa wanajilaumu wenyewe kwa kumuacha aondoke misimu kadhaa iliyopita. Amekuwa pale Bayern Munich kwa muda na alikuwa kwenye kiwango cha kuvutia kabisa.

Hata hivyo, msimu huu anaonekana kuwa mmoja wa nyota wakali zaidi. Mabao manne aliyofunga dhidi Tottenham Hotspur yanathibitisha hilo. Mjerumani huyo amekuwa kwenye kiwango kizuri zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Kama ataweza kuendelea kuwa kwenye kiwango hicho kwa wiki chache zijazo, kutamfanya kuwa mmoja wa nyota wa kuchungwa zaidi katika mashindano hayo. Tayari ana mabao manne na pasi ya moja ya mwisho katika mechi nne alizocheza msimu huu.

### 4. ERLING BRAUT HAALAND

Erling Braut Haaland yupo kwenye kiwango cha kuvutia kwa sasa. Anaweza kuwa hajulikani kwa watu wengi kwa sababu hachezi katika moja ya ligi kubwa tano za Ulaya. Anacheza pale RB Salzburg kwenye Ligi Kuu ya Austria, maarufu kama Bundesliga kama inavyoitwa ya Ujerumani. Kinda huyo anaonekana kuwa kwenye kiwango bora kabisa.

Akiwa na mabao 27 na pasi za mwisho saba kwenye mechi 20 alizocheza za mashindano yote, kijana huyo raia wa Norway hana masihara akiwa kwenye lango la goli. Na jambo la kuvutia ni kwamba tayari ana mabao nane katika mechi tano alizocheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na katika umri wake wa miaka 19, anaonekana atakuwa nyota mkali zaidi kwenye mashindano hayo msimu huu.

### 3. CRISTIANO RONALDO

Nani ambaye hamtambui? Mfalme wa Ulaya na pengine mchezaji bora wa zama hizi. Wote wanajua kwamba, Cristiano Ronaldo anaweza kuanza vibaya msimu, lakini mwishoni anakuwa moto kwelikweli.

Ronaldo ndiye mchezaji pekee aliyefunga bao katika kila mchezo wa hatua ya makundi kwenye michuano hiyo, pia ndiye aliyefunga 'hat-trick' nyingi zaidi kwenye hatua ya mtoano.

Kwa sasa Ronaldo bado hajawa kwenye kiwango, lakini wakati wowote anaweza kufanya maajabu makubwa.

### 2. LIONEL MESSI

Kumzidi mpinzani wake, Cristiano Ronaldo kwenye tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Fifa haitoshi kwake. Mara zote anataka kuwa juu ya mpinzani wake huyo raia wa Ureno.

Barcelona inakuwa kwenye wakati mgumu kama Lionel Messi hayupo kwenye kiwango chake. Bado ana maumivu ya kufungwa na Liverpool msimu uliopita.

Pamoja kwamba Messi bado hajaimarika sawasawa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, lakini ni suala la muda tu kumuona aking'ara.

### 1. ROBERT LEWANDOWSKI

Robert Lewandowski kwa sasa yupo kwenye kiwango bora zaidi na miamba wa soka wa Ujerumani, Bayern Munich. Vipi kuhusu Ligi ya Mabingwa Ulaya? Timu zilizokutana naye zinajua nini alichowafanya wakati akiwa kwenye lango la timu pinzani.

Huku tayari akiwa na mabao 10 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, ni wazi kwamba ana nafasi ya kuibuka mfungaji bora mwishoni mwa mashindano hayo.

Kwani tayari ameonyesha yupo kwenye wakati mzuri zaidi katika kipindi chake cha uchezaji na moto wake unaonekana wazi si wa kupoa hivi karibuni.

USHINDI wa mabao 5-2 Barcelona iliyoupata dhidi ya Real Mallorca kwenye LaLiga juzi, ni mechi ya tatu kwa washambuliaji Lionel Messi, Luis Suarez na Antoine Griezmann wote kwa pamoja kuweza kucheka na nyavu katika mchezo mmoja wakiwa Barca kwenye mashindano yote na wa pili kwa upande wa LaLiga (mingine ilikuwa dhidi ya Eibar na Borussia Dortmund).



NDANI YA 18

Nipashe
Spotika



LIGI Kuu ya England inachukuliwa kuwa moja ya ligi yenye ushindani mkubwa zaidi na mashabiki wengi wa soka duniani, lakini licha ya hilo si wachezaji wote bora duniani wamepata mafanikio pale.

Uk. 16&17

# MESSI NA BALLON D'OR SITA KATIKA NAMBA






**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi ameendelea kuwa na uwezo wa kutengeneza rekodi yake mwenyewe wakati aliposhinda kwa mara ya sita tuzo ya Ballon d'Or.

**Utawala wa muongo mmoja kwenye historia ya tuzo binafsi kwenye soka kati ya nyota huyo wa Barcelona na Cristiano Ronaldo ulivunjwa mwaka jana na kiungo wa Real Madrid, Luka Modric.**

Lakini tena Messi alitajwa kuichukua tuzo hiyo ya Ballons d'Or kwa mara ya sita, yaani ameshinda mwaka 2009, 2010, 2011, 2012 na 2015.

Hapa chini tunaangalia rekodi ya Messi kwa namba.

**2009**

Mwaka huu kulikuwa na mataji mengi. Alishinda mataji sita chini ya kocha Pep Guardiola akianza na taji la Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, Copa del Rey [Kombe la Mfalme], Ligi ya Mabingwa Ulaya, Supercopa de Espana, Super Cup na Klabu Bingwa ya Dunia. Messi alichangia mabao 22 na pasi za mwisho 10 kwenye LaLiga.

**2010**

Mwaka mmoja baadaye kulikuwa na mataji machache akishinda LaLiga na Supercopa, lakini ulikuwa tena mwaka wa kuvutia kwa Messi, ambaye alifunga mabao 58 katika mechi 54 alizoichezea Barcelona. Alisherehekea mabao 42 kwenye La Liga katika mechi 36.

**2011**

Kwa mara ya tatu mfululizo akashinda Ballon d'Or mwaka 2011. Taji pekee alilikosa mwaka huo lilikuwa ni lile la Copa del Rey, huku Messi akiwa na mchango mkubwa zaidi katika kikosi cha Barca kilichoshinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya. Alifunga mabao 55 katika mechi 57 alizocheza kwenye mashindano yote na pasi za mwisho 25.

**2012**

Hii ilikuwa ni mara ya nne mfululizo, wakati huo Messi alikuwa na taji moja tu la Copa del Rey. Katika mechi 60 alizocheza Messi alifunga mabao 79, huku 59 yakiwa kwenye LaLiga na 13 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na akitoa pasi za mwisho 21.

**2015**

Baada ya miaka miwili kutawaliwa na mshindani wake, Ronaldo katika tuzo za Ballon d'Or mwaka 2015 Messi akarudi tena. Akiwa na upatina mzuri na Neymar na Luis Suarez chini ya kocha, Luis Enrique alishinda taji la LaLiga, Copa del Rey na Ligi ya Mabingwa Ulaya pamoja na lile la Super Cup na taji la Klabu Bingwa Dunia. Alifunga mabao 48 na pasi za mwisho 23 katika mechi 53 alizocheza.

**2019**

Mwaka huu ndio umemtambulisha kama mchezaji bora wa wakati wote katika sayari hii. Kwani Messi ameweka rekodi ya kutwaa tuzo ya Ballon d'Or kwa mara ya sita. Mwaka huu amefunga mabao 41 na pasi za mwisho 15 katika mechi 44.

Messi pia alishinda taji la LaLiga kwa mara ya 10 akiweka rekodi ya mchezaji wa kwanza wa Barcelona kubeba taji hilo mara 10 katika historia.

**USILOLIJUA**




BAO alilofunga Alex Oxlade-Chamberlain wakati wakishinda 3-0 dhidi ya Bournemouth juzi, ni la kwanza kwake katika mechi 25 za Ligi Kuu England, alizoichezea Liverpool. Mara ya mwisho kuifungia timu hiyo ilikuwa dhidi ya Manchester City Januari 2018, mwaka mmoja na siku 327 zilizopita.





# Madarasa 59 yazuia wanafunzi 2,716 kidato cha kwanza

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAFUNZI 2,716 waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka huu na kutakiwa kujiunga kidato cha kwanza mwakani mkoani Mbeya, wako hatarini kuchelewa kuanza masomo kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa 59.

Hayo yalisemwa na Kaimu Ofisa Elimu wa Mkoa huo, George Mbigima, wakati wa kikao cha wadau wa elimu cha kutoa taarifa ya uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga kidato cha kwanza, ambapo alisema idadi hiyo ni sawa na asilimia nane ya waliofaulu.

Alisema kutokana na tatizo hilo, majina ya wanafunzi hao yamezuiliwa yasitangazwe mpaka vyumba hivyo vitakapokuwa vimekamilika, na kwamba kati ya Halmashauri saba za Mkoa huo ni Halmashauri tatu za Busokelo, Mbeya Jiji na Kyela ndizo hazina upungufu wa vyumba.

Mbijima alisema halmashauri inayoongoza kwa upungufu ni Mbarali ambayo ina upungufu wa vyumba vya madarasa 36, ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya yenye upungufu wa vyumba 11, na Halmashauri za Rungwe na Chunya zina upungufu wa vyumba sita kila moja. Aliwataka viongozi wa halmashauri hizo kuhakikisha wanasimamia ujenzi wa vyumba hivyo ili kufikia Januari viwe vimekamilika na watoto wote waanze masomo.

"Upungufu wa vyumba vya madarasa unajitokeza kila mwaka na wakati mwingine katika shule zilezile, lakini kuna shule ambazo zimefikia ukomo wa kubeba wanafunzi, hivyo nashauri halmashauri kuwa na mipango ya kujenga vyumba vipya kulingana na mahitaji pamoja na kujenga shule mpya," alisema Mbijima.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Jeremiah Minja, aliagiza halmashauri zote kukamilisha vyumba hivyo kabla ya Januari 15, ili wanafunzi wote waliozuiliwa waanze masomo mapema. Alisema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, aliagiza vyumba hivyo vikamilike kabla ya Januari 30 na hivyo wao wanatakiwa waweke tarehe ya nyuma ili kuendana na tarehe ya wizara.

Aliwataka wakuu wa wilaya, wakurugenzi na wadau wengine wa elimu katika mkoa huo kushirikiana kwenye ujenzi wa vyumba hivyo ili wanafunzi waanze mapema masomo na wauepushe mkoa na matatizo.

"Kwa kuwa Waziri Jafo aliagiza nchi nzima vyumba vikamilike mwishoni mwa Januari, sisi tutaweka katikati ya mwezi huo na kila mtu ahakikishe anashiriki kwenye zoezi hilo maana nina taarifa kuwa maeneo mengi ujenzi unaendelea," alisema Minja. Baadhi ya wakuu wa wilaya waliohudhuria kikao hicho walieleza mikakati yao ya kuhakikisha wanafunzi wote waliofaulu wanaanza masomo mapema.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema katika wilaya wameamua kujenga shule mpya tisa ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa vyumba.

Alisema kati ya shule hizo mpya, shule sita zitafunguliwa Januari, na kwamba baada ya hapo wataendelea na utaratibu wa kujenga vyumba vipya vya madarasa kwenye shule za zamani.

Alipokuwa anatoa taarifa ya wanafunzi waliochaguliwa, Waziri Jafo alisema 173,636 nchini kote wamekosa nafasi kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.



Baadhi ya wasamaria wema wakimsaidia dereva boda-boda kuinua pikipiki yake baada ya kuanguka katika eneo la Ndola Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya. Alikuwa akipanda tuta lililowekwa na wananchi, ili kudhibiti mwendokasi wa madereva hao. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Watatu mbaroni kwa tuhuma za mauaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU watatu wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kwa tuhuma za mauaji ya John Mwakarundwa (62), Mkazi wa Kijiji cha Nkunga katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe tukio ambalo linahusishwa na imani za kishirikina.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema tukio hilo lilitokea Desemba 3, majira ya jioni kijijini hapo, ambapo watuhumiwa walimvamia na kumkata na vitu vyenye ncha kali. Kamanda Matei alisema majina ya watuhumiwa hao yanahifadhiwa kwa sababu za kiuchunguzi, na kwamba walimkatakata Mwakarundwa maeneo ya kisogoni, taya la kushoto na tumboni hali iliyosababisha kifo chake. Alisema historia inaonyesha kuwa Mwakarundwa alikuwa anatuhumiwa kwenda kununua uchawi Malawi, hivyo wananchi wa eneo hilo walikuwa wana hasira naye wakidai alikuwa anawatesa kijijini hapo. Alisema watuhumiwa wanadaiwa kufanya tukio hilo kwa lengo la kulipiza kisasi, na kwamba baada ya tukio hilo wananchi walikuwa wanashangilia wakifurahia kuuawa kwake.

"Serikali haiwezi kujiingiza kwenye hizo imani za kishirikina, hivyo tutaendelea kuwahoji watuhumiwa, na ushahidi ukikamilika watafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria," alisema Kamanda Matei.

# Fursa ya umeme vijiji 140

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIJIJI 140 vya Mkoa wa Mbeya vimeunganishiwa huduma ya umeme kupitia Wakala wa Huduma za Nishati Vijijini (REA), awamu ya tatu, hivyo kurahisisha upatikanaji wa baadhi ya huduma za kijamii na kuinua uchumi wa wananchi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco) Mkoa wa Mbeya, Shamu Lameck, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusu utekelezaji wa mradi huo.

Shamu alisema REA awamu ya tatu mzunguko wa kwanza unatekelezwa katika wilaya zote kupitia mkandarasi Steg International Service kutoka Tunisia.

Alisema utekelezaji wake ulianza Mei 2018 na unatekelezwa kwa miezi 24, na kwamba utekelezaji wake umegawanyika katika mafungu mawili, ambapo kila fungu lina halmashauri tatu.

Kwa mujibu wa Shamu, fungu la kwanza linajumuisha Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Busokelo na Rungwe ambapo katika fungu hilo vijiji 110 vipo kwenye mradi, vikiwamo vya wilaya za Ileje na Mbozi mkoani Songwe.

"Mradi huu unagharimu Sh. bilioni 25.4 na ni mradi wenye manufaa makubwa kwa wananchi, sasa hivi baadhi ya vijiji, na vimewashiwa umeme... kuna shughuli za kiuchumi zimeongezeka, watu wanachomelea, wanachaji simu na miradi mingine," alisema Shamu.

Alisema fungu la pili linajumuisha Halmashauri za Wilaya ya Chunya, Kyela na Mbarali pamoja na vya Wilaya za Momba na Songwe mkoani Songwe ambapo vijiji na vitongoji 58 vitanufaika na unagharimu Sh. bilioni 20.5.

Alisema utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 49, na kwamba wanatarajia mkandarasi atakamilisha kazi hiyo kwa muda wa kipindi ambacho kimeainishwa kwenye mkataba.

Akizungumzia changamoto za mradi huo Shamu alisema baadhi ya wananchi wanakuwa wagumu kuridhia miundombinu ya umeme kupita kwenye maeneo yao pamoja na mwamko mdogo wa kuunganisha umeme kwenye maneo ambayo mradi umepita.

"Katika awamu hii tulilenga wateja 7,549 wawe wameunganishiwa umeme na hilo tumefanikiwa, lakini pia tumefanikiwa kufunga transifoma 168 katika mtandao wa umeme vijijini wenye urefu wa kilomita, 332," alisema.

Aliwataka wananchi kulinda miundombinu ya REA, ambayo imeegeshwa au kusimikwa kwa ajili ya kupitisha mradi wa umeme okiwamo kukubali kupisha miundombinu hiyo ipite katika maeneo yao ili serikali ikamilishe kazi hiyo haraka kwa ajili ya maendeleo yao.



# Osha yatoa somo kwa mafundi

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

KAIMU Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (Osha), Khadija Mwenda, amewataka mafundi katika nyanja mbalimbali kuongeza thamani ya kazi zao ili waweze kujiinua kiuchumi kutoka kipato cha chini hadi cha kati.

Aliyasema hayo wakati wa kongamano la mafundi lililofanyika jijini hapa na kueleza kuwa mafundi wana mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi hususani kufanikisha Tanzania ya viwanda.

"Kwa miaka mingi kumekuwa na dhana iliyojengeka ndani ya jamii zetu kwamba mafundi ni watu wa chini na wenye mchango mdogo katika maendeleo ya nchi; dhana ambayo haina ukweli wowote. Hivyo, nawaasa mafundi kuanza kujiona kuwa watu wenye thamani sana na wenye mchango mkubwa katika maendeleo ya familia, jamii na taifa kwa ujumla," alisema Mwenda. Kadhalika, aliwasisitiza mafundi kuhusu uzingatiaji wa kanuni muhimu za kujilinda dhidi ya vihatarishi vya kiusalama na afya wanapokuwa wanafanya kazi zao za kiufundi.

"Mara nyingi tunapofikiria maendeleo tunadhani yanaletwa na shughuli kubwa za kiuchumi tu mfano viwanda vikubwa na kusahau kwamba ni viwanda vidogo na wazalishaji wa chini ndio hupeleka malighafi katika viwanda vikubwa," alisema Mwanda.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Kampuni ya Fundismart iliyoandaa kongamano hilo, Wiseman Luvanda, ambaye ni Meneja Mradi wa kampuni hiyo, alisema programu ya FundiSmart ina lengo la kuwawezesha mafundi kutumia ujuzi na vipaji vyao ipasavyo ili waweze kupata mafanikio na kuboresha maisha yao.

Katika kongamano hilo washiriki walipata mafunzo mbali mbali yakiwamo ya usalama na afya mahali pa kazi ambayo yalitolewa na Mkaguzi wa Usalama wa Mazingira ya kazi kutoka Osha, Venance Bulinga.



Mariam Ngizo (kushoto) na Philipina Kobelo wote kutoka Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Watumishi wa Umma Ofisi ya Rais, wakitoa mafunzo kwa viongozi wa serikali katika kitongoji cha Nyerere kilichopo Kijiji cha Buigiri Wilaya ya Chamwino.
**PICHA PETER MKWAVILA.**

# Makandarasi wazawa wapigiwa debe zabuni Tanroads, Tarura

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameawaagiza Wakala wa Barabara (Tanroads) na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (Tarura) kuhakikisha wanatoa kazi kwa makandarasi wazawa ambao wana uwezo wa kufanya kazi za kujenga barabara na madaraja mkoani humo.

Akizungumza baada ya kukagua daraja la Ibwaga wilayani Kongwa ambalo limejengwa na Mkandarasi Tactics and Construction Company, Thobias Kyando, Mahenge alisema mkandarasi huyo ameonyesha uwezo wa juu katika kujenga daraja ambalo limefikia asilimia 92.

Dk. Mahenge alisema mkandarasi huyo ameonyesha uwezo wa juu katika kujenga daraja katika mto huo ambao mara mvua zikinyesha wananchi kutoka Mlalo inawawia vigumu kufika katika hospitali ya wilaya kupata huduma za afya.

Alisema mara nyingi miradi ya barabara wamekuwa wakipewa makandarasi kutoka nje, lakini hawafanyi vizuri, na kuongeza kuwa Kyando ni mfano wa makandarasi wazawa ambao wameonyesha uwezo wa juu katika kujenga daraja.

Mahenge alisema kutokana na uwezo alionyesha kujenga daraja hilo, ni vema Tanroads kumtumia katika kazi ujenzi wa miradi mingine kwani amejenga sifa kutokana na kujenga daraja hilo.

Alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Deogratus Ndejembi, kuhakikisha katika kampeni yao ya kupanda miti, wananchi wa maeneo hayo wafike kwenye kingo za daraja hilo na kupanda minyaa kuzuia mmomonyoko.

Awali, Ndejembi alisema eneo hilo lilikuwa sugu halipitiki wagonjwa wengi kutoka Kata ya Mlali walikuwa wakipata taabu kupata huduma katika hospitali ya wilaya na wakati mwingine walihitaji watu wa kuwabeba kuwavusha.

Naye Mkandarasi Kyando alisema daraja hilo lenye urefu mita 51 na upana mita 13 na midomo ya kupitia maji minane, limetumia Sh. bilioni 2.19 na ujenzi wake umefikia asilimia 92 litakamilika Januari 4, 2020 kwa kuweka vyuma vya kukinga wapita kwa miguu wasianguke wanapovuka ambavyo tayari ameviagiza.

Mmoja wa mwananchi wa Ibwaga, Prisca Mahimbi, alisema daraja hilo ni ukombozi wa wanawake na watu wengine kwa kuwa watakuwa wanavuka wakati wa masika ambapo awali walilazimika kuahirisha safari kutokana na kushindwa kuvuka.

# Watumishi 2,000 Takukuru wakosa nyumba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) nchini inakabiliwa na uhaba wa nyumba za watumishi zaidi 2,000.

Hayo yalibainishwa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali John Mbungo, katika mkutano wa mwaka wa taasisi hiyo.

Alisema taasisi hiyo inamiliki nyumba 13 nchi nzima wakati mahitaji yao ni zaidi ya nyumba 2,000.

Mkurugenzi huyo alisema uhitaji wa nyumba ni muhimu kutokana na watumishi wengi wanaishi nyumba za kupanga.

"Tunaomba Waziri Mkuchika (George) uliangalie hilo moja ya changamoto tunayokumbana nayo ni uhaba wa makazi ya watumishi, " alisema Brigedia Mbungo.

"Pia tunakabiliwa na uhaba wa watumishi, ambapo waliopo ni 2,100 badala ya 4,000 kama muundo mpya wa Takukuru unavyotaka," alisema.

Kuhusu utendaji kazi, Mbungo alisema wamekuwa wakitoa mada kuhusu namna bora ya kudhibiti vitendo vya rushwa mahala pa kazi kwenye taasisi mbalimbali nchini.

Alisema hali hiyo imesaidia kwa kiasi kikubwa kuwapa uelewa watumishi namna ya kujiepusha na vitendo vya rushwa katika utendaji kazi wao wa kila siku.

"Mialiko tunayopata kwa ajili ya kutoa mada inasaidia kwa kiasi kikubwa kuielimisha jamii, tumekuwa tukitumia pia vyombo vya habari kuelimisha umma kupitia mada za rushwa, " alisema Mbungo.

Alisisitiza taasisi hiyo itaendelea kuwaelimisha kuhusu suala la kujiepusha na kutoa au kupokea rushwa jambo ambalo ni kinyume na kifungu cha sheria.

Alisema katika utekelezaji wao wamechukua hatua mbalimbali kuimarisha utendaji kazi wao ikiwamo kufanya majadiliano na waendesha mashtaka kuhusu changamoto zinazojitokeza mahakamani kupitia hati za mashtaka kabla ya kufungua kesi na kuandaa "prosecution plan".

"Hii imesababisha kati ya kesi 1003 zilizoendeshwa mahakamani kesi 341 zilizotolewa uamuzi na kati ya hizo tumeshinda kesi 206 sawa na asilimia 60.41," alisema.

Aidha, alisema usimamizi wa maadili na uadilifu umeimarishwa ngazi zote na kuongeza kuwa wataendelea kufuata maadili ya kazi.





# 145 wafariki dunia ajali barabarani miezi 10

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

AJALI za barabarani zinaendelea kutishia maisha ya wananchi Zanzibar hasa wakati huu ambao serikali ikiendelea na uimarishaji wa miundombinu ya barabara na mitaro ya maji ya mvua.

Takwimu za hivi karibuni visiwani Zanzibar, zimebainisha kwamba watu 145 wamepoteza maisha kutokana na ajali za barabarani kuanzia Januari hadi Oktoba mwaka huu.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, alisema ni jambo la kuhuzunisha kuona kwamba utafiti unaonyesha kuwa watu 12 hufariki kila mwezi kutokana na ajali za barabarani.

Alisema ajali hizo zimekuwa zikiripotiwa kila siku na kuacha majonzi na simanzi kwa wananchi.

Balozi Iddi alisema hiyo ni hali ya kutisha na umefika wakati wa kuchukuliwa hatua madhubuti za kudhibiti ajali barabarani ikiwamo kuhakikisha mtu asiye na leseni ya udereva haendeshi chombo cha moto.

Aliliagiza Jeshi la Polisi kuwadhibiti watu wanaoendesha vyombo vya moto wakiwa wamelewa.

"Ni vyema Jeshi la Polisi kusimamia vilivyo matumizi ya alama za barabarani na yule atakayekiuka taratibu hizo, lazima aadhibiwe kwa mujibu wa sheria," alisema.

Alisema adhabu zinapaswa pia kuwageukia watu wanaojaribu kutaka kujiua wenyewe kwa njia tofauti ikiwamo kula dawa au sumu na wengine hujaribu kujinyonga kwa kutumia kamba au nguo.

Alisema hilo ni wimbi jipya la masuala ya udhalilishaji na unyanyasaji linaloendelea kuwa janga la dunia ambalo kwa sasa linaonekana kuibuka na kuleta athari Zanzibar.

Balozi Iddi alitahadharisha na kuikumbusha jamii kwamba sheria za nchi zinatambua kuwa tendo la kutaka kujiua ni kosa la jinai.



Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idrisa Muslim Hija, akizungumza na walimu wa shule mbalimbali zilizopata ruzuku za ufaulu wa juu katika ukumbi wa Jamhuri Wete Pemba **(PICHA NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR)**.

# SMZ yawataka wawekezaji kulipa kodi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, imewataka wawekezaji kutimiza wajibu wao wa kulipa kodi ili kwenda sambamba na dhamira ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuimarisha sekta ya utalii.

Akizungumza juzi katika hafla ya kutunuku zawadi kwa wawekezaji waliofanya vizuri zaidi mwaka huu baada ya maonyesho ya utalii yaliyofanyika Septemba mwaka huu Mjini Zanzibar, Waziri wa wizara hiyo, Mahmoud Thabit Kombo, alisema suala la kodi halina mjadala.

Waziri Kombo alisema utalii kwa sasa ndio sekta mama ambayo serikali inaitegemea zaidi kuingiza mapato kwa ajili ya kazi za maendeleo na ustawi wa jamii.

Alisema hoteli inapotoa huduma ya malazi kwa upendeleo maalum na kusamehe malipo, ofa hiyo isiwe sababu kwa mwekezaji kudai kuondolewa kodi ambayo ni lazima ilipwe.

"Naomba tuige mfano wa mashirika ya ndege ambayo hata yanapotoa tiketi ya bure kwa abiria, kodi inayotokana na kiti alichopewa msafiri inalipwa. Kodi unayolipa ndio inayojenga shule atakayosoma mtoto wako, inanunua dawa zako na wananchi wote," alieleza.

Alieleza kuwa haja kwa wawekezaji na wafanyabiashara zinazohusiana na sekta ya utalii na nyingine, kutimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa hiari, na kuacha ukaidi unaosababisha kukimbizana na mamlaka za kukusanya mapato na kusababisha miradi yao kufungwa.

Aliwapongeza wote waliotwaa tuzo ya utendaji mzuri, na kutaka fursa hiyo iwe kichocheo cha kukuza biashara zao.

Alisema takwimu za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) zinaonyesha kuwa asilimia 30 ya pato la serikali ambayo ni dola milioni 476 (zaidi ya Sh. trilioni moja) zinatokana na sekta ya utalii, na hicho ni kielelezo kwamba wawekezaji wanafanya kazi kubwa ambayo serikali inaithamini na kwa hivyo ikaona iko haja ya kuwaandalia tuzo maalumu.

Naye Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Dk. Abdalla Mohammed Juma, alisema utaratibu wa kuwazawadia wawekezaji wa sekta ya utalii, unalenga kukuza azma ya serikali kufanya kazi kwa karibu na sekta binafsi kwa manufaa ya pande zote pamoja na kufikia lengo la utalii kwa wote.

Alisema kuimarika kwa utalii wa Zanzibar kunaonekana wazi katika ongezeko la watalii wanaofika nchini, ambapo hadi mwezi wa Desemba 2018, jumla ya wageni 527,000 walitembelea visiwa hivyo.

Hafla hiyo ilidhaminiwa na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF).

Kamishna wa ZRB, Joseph Abdalla Meza, alisifu mchango mkubwa unaotolewa na sekta ya utalii, huku akiwapongeza wawekezaji walio wengi kwa kulipa kodi kwa wakati na kwa usahihi. Alisema si vyema baadhi ya wawekezaji kufanya udanganyifu katika kodi zao, na kuwataka wenye tabia hiyo kutii sheria ili serikali iweze kukusanya mapato ambayo ndiyo yanayotumika kwa maendeleo ya wananchi.

Sabra Issa Machano, Mkurugenzi Mtendaji wa ZSSF, alisema michango ya sekta binafsi hasa hoteli za kitalii kuwalipia wafanyakazi wao, imeimarisha mfuko huo na kuwezesha kufanya miradi mbalimbali mikubwa.

# Walimu wahimizwa kufundisha

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idrisa Muslim Hija, amewataka walimu wa shule za msingi na sekondari kuzidisha ari ya kufundisha ili kukuza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi.

Akizungumza jana katika sherehe maalum ya utoaji wa ruzuku ya ufaulu iliyofanyika Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba, Dk. Idirisa, alisema hatua hiyo itasaidia pia kupata wataalamu wengi.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia mradi wa ZISP, imetoa fedha za kwa lengo la kuzifanya shule ziweze kufaulu zaidi.

Alisema katika kufikia malengo hayo, ni lazima walimu kujiandaa pamoja na wanafunzi wao kwa kuongeza juhudi za kusoma pamoja na wazazi kuchangia katika maendeleo ya elimu kwa watoto.

Aliwataka walimu kutumia zawadi hizo kwa kununua vifaa mbalimbali vikiwamo vya maabara, samani na marekebisho madogo ya ujenzi wa shule ili kuweka mazingira mazuri ya kufundisha na kujifunza.

Aidha, aliwataka walimu kutimiza majukumu yao ya kila siku katika kazi na kuwaonya juu ya kutotimiza ipasavyo majukumu hayo kwa kutokufika shule.

Naye Ofisa Mdhamini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba, Mwalim Mohammed Nassor Salim, alisema lengo la serikali la kuzizawadia shule 100 katika kila ngazi halikufikiwa kwa mwaka 2018, hivyo ana matumaini kuwa kwa mwaka huu zinaweza kupita.

Mohammed aliwataka walimu wa shule zitakazopatiwa zawadi hizo kuzitumia kama ilivyokusudiwa wakitambua kuwa taasisi za ukaguzi na ufuatiliaji zitapita.

Kwa upande Mkuu wa Wilaya ya Wete Pemba, Kapteni Khatib Khamis, aliwapongeza walimu wakuu kwa kufanikisha kupata matokeo bora katika shule zao.

# Mil. 176/- kujenga vyumba vya madarasa

**Na Hamisi Nasiri,**
TANDAHIMBA

WILAYA ya Tandahimba mkoani Mtwara imetenga Sh. milioni 176 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa vitakavyotumika kusomea wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka 2020.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Sebastian Waryuba, wakati wa kikao cha kutangaza matokeo ya majina ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mkoani Mtwara, ambacho kilihusisha wadau wa elimu mkoani humo.

Alisema Wilaya ya Tandahimba imefanikiwa kufaulisha wanafunzi kwa asilimia 83, na kwamba hayo ni mafanikio makubwa kitaaluma ukilinganisha na kipindi cha miaka ya nyuma ya 2018/219, ambapo wilaya hiyo ilikuwa nyuma kitaaluma.

Alisema Wilaya ya Tandahimba kwa mwaka 2020 imefanikiwa kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi ambao wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza.

Alisema wanafunzi ambao walifanya mtihani wa darasa la saba 2019 katika Wilaya ya Tandahimba ni 5,630 na walifaulu kujiunga na kidato cha kwanza ni 4,601.

Alisema kwa matokeo hayo Wilaya ya Tandahimba inakuwa imefaulisha kwa asilimia 83 kwa mwaka 2019 kwa wanafunzi wanaojiunga elimu ya sekondari kidato cha kwanza mwaka 2020.

"Tunawaomba wazazi hizo fedha za korosho wanazozipata wajiandae kuwapatia watoto wao mahitaji ya msingi ya shuleni, na sisi serikali ujenzi wa vyumba vya madarasa tutaukamilisha kwa wakati ili wanafunzi hawa wasome," alisema Waryuba.

Waryuba alisema licha ufaulu huo wilaya ya Tandahimba kwa sasa ina changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa 14.

Alisema kwa kuliona hilo, serikali imetenga Sh. milioni 176 kwa ajili ya kujenga vyumba vya madarasa ili kuondoa tatizo hilo.

Aidha, Mkuu huyo wa Wilaya, amewata wazazi na walezi wilayani humo ambao watoto wao wamechaguliwa kuendelea na masomo ya sekondari kutumia vizuri fedha zao za malipo ya korosho katika kuwaandalia mahitaji ya msingi ya shuleni.

Ofisa Elimu Mkoa wa Mtwara, Germans Mung'aho, alisema mkoa wa Mtwara umekuwa ukifaulisha vizuri mwaka hadi mwaka, na kwamba mwaka 2020 wanafunzi ambao wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza ni 22,810.

Katibu Tawala Mkoa wa Mtwara, Alphayo Kidata, amewapongeza wanafunzi wote wa mkoani Mtwara ambao wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza na kwamba ni jukumu la wazazi kuhakikisha watoto hao wanaendelea na masomo yao ya sekondari.




Mkuu wa Hazina na Masoko ya Mitaji wa BancABC, Briton Mwasamengo (kulia), akihojiwa na mtangazaji wa East Africa Radio Ian Dialo katika kampeni ya "Kibiashara Zaidi" ya EATV, ambapo alieleza kuwa benki hiyo inatoa huduma zote za kibenki ikiwamo utoaji wa mikopo kwa wateja wakubwa na wadogo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahitimu vyuo vikuu watakiwa kujiajiri

**Na Mary Geofrey**

WAHITIMU wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, wametakiwa kutumia taaluma waliyopatiwa katika kujiajiri badala ya kuzunguka mtaani na bahasha za vyeti vya taaluma kutafuta kazi

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Lughano Kusiluka, wakati wa sherehe za mahafali ya 18 tawi la Dar es Salaam.

Alisema hatarajii kuona wahitimu wa chuo hicho wakizunguka na bahasha zenye nakala ya vyeti wakitafuta kazi wakati wamejengewa uwezo na ujuzi wa kujiajiri na kusaidia serikali katika kufikia azma ya kukuza uchumi wa Taifa ifikapo 2025.

"Kwa fani ambazo mmezisomea hapa chuoni, ni dhahiri kwamba mmepata elimu, ujuzi na maarifa ya kutosha ya kushiriki kwenye ajenda hii muhimu ya kitaifa. Hutataki wahitimu wa Mzumbe wazunguke na bahasa yenye nakala za vyeti kutafuta ajira," alisisitiza Prof. Kusiluka.

Naye Kaimu Mwenyekiti wa Baraza chuo hicho, Pius Maneno, aliwataka wahitimu hao kutumia elimu na ujuzi waliopata kutatua changamoto zinazoikabili jamii sambamba na kuwa wabunifu.

"Kuhitimu kwenu mnakuwa sehemu ya nguvu ya kazi ya Taifa letu, jamii ya Watanzania inawategemea kwa elimu, ujuzi weledi na maarifa mliyoyapata chuoni. "Tunaamini mtaleta mabadiliko chanya katika maisha yenu, familia na jamii zitakazowazunguka," alisema Maneno.

Katika mahafali hayo jumla ya wahitimu 445 walitunukiwa shahada za umahiri wa fani mbalimbali kati ya hao wanawake 236 sawa na asilimia 53.0 na wanaume 209 sawa na asilimia 47.

Baadhi ya wanafunzi waliohitimu, walisema idadi ya wahitimu imekuwa kubwa kulinganisha na nafasi za ajira zinazotolewa, hivyo kumewafanya wajiandae kisaikolojia kujiajiri.

Rais wa Serikali ya Wanafunzi aliyemaliza muda wake, David Lema, alisema chuo hicho kimewapa mafunzo ya ujasiriamali wa taaluma yao hivyo wataenda kuutumia ujuzi huo ili kuajiri vijana wengine.

# Machinga walia usafi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAFANYABIASHARA wadogo wa vyakula waliopo eneo la Bandarini mkoani Kisiwani Pemba, wamelalamikia hifadhi ya biashara zao, na hali ya usafi wa maeneo wanayofanyia biashara.

Wakizingumza na wanahabari, walisema licha ya kutozwa mapato kila siku, hali ya eneo la biashara si salama kutokana na kutofanyiwa usafi kwa wakati.

Fatma Nassor Ali, mfanyabiashara wa samaki wa kukaanga, alisema licha ya changamoto nyingi walizonazo, kubwa zaidi ni kukosa sehemu maalumu ya hifadhi biashara zao wakati wa mvua.Alisema kipindi cha mvua kinahitaji usalama wa biashara kuepukana na maradhi ya kuambukiza.

"Sisi wafanyabiashara tunajitahidi kuweka usafi wa biashara zetu, lakini kama maeneo yatakuwa hayaridhishi si letu hilo ni la Baraza la Mji wenyewe maana pesa ya usafi tunalipa," alisema.

Siti Mtumwa Ali, mfanyabiashara wa maandazi, alisema ucheleweshaji wa uzolewaji wa taka katika eneo hilo unaweza kusababisha matatizo licha biashara hizo ziko kwenye visanduku.

Alisema katika utunzaji wa biashara zao wanafuata maelekezo ya Baraza husika ikiwamo kutengeneza visanduku na kufunika vizuri, ingawa bado usafi katika maeneo ya kuuzia biashara haujiimarisha.

Muuza kahawa, Ali Omar Abdallah, alisema pia ukosefu wa vyoo katika eneo hilo unawasababishia watu wanaofika hapo kujisaidia ovyo, jambo ambalo linasababisha uchafuzi wa mazingira hasa kwa wafanyakazi wa maandazi na chapati.

Naye Ofisa wa Afya wa Baraza la Mji, Bimkubwa Haji Makame, alisema: "Sisi kabla ya mfanyabiashara hajaanza shughuli zake za biashara huwa tunampa maelekezo juu ya kuweka usafi wa biashara zao ili kuepukana na maradhi ya milipuko kama kipindu pindu." Mkurugenzi wa Baraza la Mji Mkoani, Rashid Abdallah Rashid, alisema eneo linalofanyiwa biashara na wafanyabiashara hao wadogo sio rasmi na baraza linajiandaa kuwawekeza wafanyabiashara hao eneo rasmi huko Ng'ombeni.

Kuhusu vyoo alisema: "Vyoo katika eneo hilo vipo vinne na tunawataka wananchi wavitumie, ili kuweka usafi wa mazingira katika eneo hilo lenye mkusanyiko wa watu."

## HABARI KIMATAIFA

# Moto wateketeza kiwanda, 40 wafariki

**NEW DELH,** India

MOTO mkubwa ulioteketeza kiwanda cha mabegi katika Mji Mkuu wa India Delhi, umewaua wafanyakazi 43.

Taarifa zinaeleza kuwa moto huo ulizuka katika nyumba ya ghorofa nne katika eneo la kale la makazi lenye msongamano jana asubuhi.

Watu takribani 100 walikuwa wamelala ndani ya kiwanda hicho, ambacho hutengeneza mabegi ya shule, wakati moto huo ulipoanza, lakini zaidi ya watu 60 wameokolewa.

Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi, ametaja tukio hilo kuwa la kusikitisha na kutuma salamu zake za rambirambi kwa walioathiriwa.

**Nilipigiwa simu na rafiki yake kunifahamisha kuwa amejeruhiwa katika mkasa huo. Sina habari amepelekwa hospitali gani.**

Moto huo ulianza katika vyumba vya chini vya jengo hilo na kusambaa hadi ghorofa ya tatu ambapo wafanyakazi walikuwa wanalala.

"Niliamshwa na kelele za watu wanaoomba msaada, niliona watu wamekwama ndani. Tuliwashauri wapande juu ya paa la nyumba ili tuweze kuwasaidia, lakini hawakuweza kufanya hivyo," alisema Ronak Khan, mwenye umri wa miaka 17, anayeishi nyumba ya jirani lilipotokea tukio.

Eneo ambalo kiwanda hicho kipo ni karibu na soko la Azad, ambako njia ni nyembamba, hali iliyowapa wazima moto changamoto ya kufikia.

Waokoaji walilazimika kuwabeba majeruhi mabegani mmoja baada ya mwingine.

Hata hivyo, bado haijafahamika chanzo cha kutokea kwa moto huo, lakini agizo la kufanyika kwa uchunguzi kufanywa limetolewa. Mmoja wa mashuhuda alieleza kuwa hitilafu za umeme huenda ikawa ndiyo chanzo.

Watu kadhaa waliojeruhiwa katika mkasa huo kwa sasa wanapatiwa matibabu katika hospitali tofauti mjini humo.

Ndugu, jamaa na marafiki wa waathiriwa wa tukio hilo wamekuwa wakitafuta taarifa kuhusu hatima ya wapendwa wao. Mtu mmoja ameliambia Shirika la PTI nchini India kuwa ndugu yake alikuwa ndani ya jengo hilo.

"Nilipigiwa simu na rafiki yake kunifahamisha kuwa amejeruhiwa katika mkasa huo. Sina habari amepelekwa hospitali gani," alisema.

Miji ya India imekuwa ikikabiliwa na visa vibaya vya moto, huku mpangilio mbaya wa makazi na kuzembea kwa maofisa katika suala la kuzingatia kanuni za usalama kama chanzo kuu cha mkasa huo. **BBC**



Waokoaji jijini Nairobi wakiwa katika uokoaji baada ya jengo lenye ghorofa sita kuporomoka jijini humo, nchini Kenya, watu kadhaa wanahofiwa kufunikwa na vifusi vyake. **PICHA ALLIANCE**

## Mafuriko yaacha simanzi, huzuni

**KAMPALA,** Uganda

WATU 12 wamepoteza maisha katika Wilaya ya Bundibugyo nchini Uganda baada ya kusombwa na maji, kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha na kusababisha mafuriko makubwa.

Shirika la Msalaba Mwekundu nchini humo, limethibitisha kupata miili ya watu hao ndani ya maji siku ya Jumamosi, kutokana na mafuriko hayo ambayo yameharibu pia miundombinu kama barabara.

Hali kama hiyo pia imekuwa ikishuhudiwa nchini Kenya na baadhi ya maeneo nchini Tanzania.

Wataalamu wa hali ya hewa wanasema kuwa, eneo la Afrika Mashariki litaendelea kupokea mvua kubwa katika siku zijazo na kutoa wito kwa watu kuchukua tahadhari.

Maofisa nchini Kenya wanasema watu zaidi ya 120 wamepoteza maisha kutokana na mafuriko hayo makubwa ambayo yamewaacha watu wengine 160,000 bila makazi.

Hali ilikuwa mbaya sana katika Jimbo la Pokot Magharibi kutokana na athari ya mafuriko hayo.

Nchini za Burundi, Sudan, Djibouti, Ethiopia na Somalia pia zimeendelea kushuhudia mvua kubwa iliyosababisha mafuriko na maafa. **RFI**

## Korea yamwita Trump mzee mwenye akili iliyodhoofu

**PYONGYANG,** Korea Kaskazini

KOREA Kaskazini imemwita Rais wa Marekani, Donald Trump kwamba ni mzee mwenye akili iliyodhoofu.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Korea Kaskazini, Ri Yong Hon, alisema kwamba Rais Trump (pichani) ni mchokozi na kwamba anafaa kuchunguzwa akili.

Korea Kaskazini iliwahi kumwita Rais Trump mzee aliyedhoofika kiakili mwaka 2017, na imerudia kauli hiyo tena. Ni mara ya kwanza baada ya kipindi cha mwaka mmoja kwamba Pyongyang imekuwa ikimkosoa Rais Trump waziwazi.

Kamusi ya Oxford inaelezea neno Dotard kama mtu ambaye akili yake imedhoofika hususani mzee ambaye uelewa wake umedhoofika.

Dotage inaelezewa kuwa kutokuwa na uelewa katika miaka ya uzeeni ama kwa matumizi ya jumla kama umri wa uzeeni.Wawili hao walifanya mazungumzo ya ana kwa ana nchini Singapore Juni 2018 na Vietnam mnamo Februari mwaka huu yanayolenga kusitisha mipango ya kinyuklia ya taifa hilo.



Lakini mazungumzo yamekwama tangu wakati huo, na licha ya mkutano mwingine kufanyika katika eneo la mpakani linalozigawanya Korea Kaskazini na Korea Kusini Juni mwaka huu, upande wa Kaskazini ulianza tena kufanyia majaribio makombora ya masafa mafupi.

Pyongyang imeipatia Washington muda wa mwisho kutoa mapendekezo yake ya mwisho wa mwaka kuhusu mipango yake ya kinyuklia, ikisema kuwa itatoa mwelekeo mpya iwapo hilo halitafanyika. Katika mkutano wa Nato nchini Uingereza mwanzoni mwa wiki hii, Rais Trump alimtaja kiongozi wa Korea Kaskazini. Kim Jong Un kama 'rocket man'. Rais Trump aliongezea kwamba Marekani ina kila uwezo wa kutumia nguvu za kijeshi dhidi ya Pyongyang.

Katika taarifa iliotolewa na chombo cha habari cha Korea Kaskazini, Makamu wa Rais, Choe Son Hui alionya kwamba vita vya maneno vilivyoanza miaka miwili iliyopita huenda vikaanza upya.

Alisema iwapo lugha yoyote ama maneno yanayoweza kuchafua mazingira yaliyopo yatatumika kwa lengo fulani na katika wakati muhimu, hiyo itachukuliwa kama akili ya mtu mzee iliyodhoofika.

Mwaka 2017, viongozi hao wawili walikabiliana kimaneno huku Rais Trump akimuita Kim kama mtu mdogo "little rocket man" na mwendawazimu huku naye Kim akimuita rais huyo wa Marekani mtu ambaye akili yake ni punguani. **BBC**

# Ireland kusaidia Tanzania mapambano ukatili kijinsia

**Na Joseph Mwendapole**

UBALOZI wa Ireland nchini umetoa wito kwa Watanzania kuchukua hatua kuwalinda waathiriwa wa vitendo vya ubakaji na ukatili wa kijinsia na kwamba nchi yake iko tayari kusaidia jitihada za serikali na asasi za kijamii (CSO) ili kufikia malengo hayo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Balozi wa nchi hiyo, Paul Sherlock, kwenye mdahalo wa kitaifa wa namna ya kuimarisha mfumo wa haki jinai, ulioandaliwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Africa (WiLDAF).

Alisema Ireland itaendelea kusaidia jitihada za serikali na asasi zisizo za kiraia (CSOs) katika mapambano dhidi ya ukatili wa wanawake na watoto na kuhakikisha waathiriwa wa vitendo hivyo wanalindwa na sheria zilizopo.

Alisema kuna umuhimu wa kuimarisha mfumo wa utoa wa taarifa za unyanyasaji wa kijinsia, uchunguzi na uendeshaji wa mashtaka ya aina hiyo kwa kuwajengea uwezo wahusika wanaosimamia kesi za ukatili wa kijinsia.

Balozi alisema kutokana na sababu mbalimbali matukio ya ukatili hayaripotiwi hali ambayo inahatarisha afya na utu wa waathiriwa wa vitendo hivyo na kwamba hata kesi zinazofikishwa mahakamani ni chache sana.

"Nchini kwangu tunakabiliwa na matatizo kama haya na utafiti wa mwaka 2014 ulibaini kuwa asilimia 79 waliofanyiwa ukatili na wenza wao hawakuwahi kutoa taarifa kwenye vyombo vya dola na badala yake wanarudi nyumbani walikofanyiwa ukatili huo," alisema.

Alisema ubalozi huo umekuwa ukisaidia harakati za usawa wa kijinsia, kupinga ukatili wa kijinsia na kujenga uwezo kwa mfumo wa utoaji haki ili wahusika watendewe haki.

Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Nyanda Shuli, alisema wahusika wa matukio mengi ya ubakaji na ukatili wa kijinsia wanafikishwa mahakamani.




Balozi wa Norway nchini Tanzania, Elisabeth Jacobsen, akizungumza na wageni waalikwa jijini Dar es Salaam jana, kwenye mahafali ya tano kwa wahitimu 14 waliofadhiliwa kusoma na kampuni ya Equinor Tanzania kwa kiwango cha Shahada ya Uzamili katika masomo ya Petroleum Geosciences, Petroleum Engineering na Project Management Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wengine ni Prof. Ulingeta Mbamba wa UDBS, Meneja Mkazi wa Equinor Tanzania, Dk. Mette Halvorsen Ottøy, Prof. Egil Tjland wa NTNU, Prof. Prof. Jon Kleppe wa NTNU na Mwakilishi wa Bodi ya Norad, Erik Holtar. **NA MPIGAPICHA WETU**

# NMB yatwaa tuzo NBAA mwaka wa pili

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB, imetwaa Tuzo Maalum kutoka Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (NBAA), kama Benki Bora ya Taarifa za Kifedha zilizokaguliwa na kutambuliwa kimataifa kwa mwaka 2019, ilikozishinda benki kadhaa nchini.

Hafla ya kukabidhiwa tuzo hiyo ambayo kwa NMB, ni ushindi wa mara ya pili mfululizo, ilifanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ambako NBAA ilisema taarifa za kibenki za NMB zimeendelea kuwa bora kila mwaka, ubora uliowasukuma majaji kuwapa tuzo hiyo.

Tuzo hiyo, ni kipimo cha ubora wa taarifa za kifedha miongoni mwa kampuni mbalimbali, ambao hupitia katika mfumo bora wa ukaguzi na uchunguzi unaosimamiwa na majaji wazoefu, unaojumuisha kampuni zinazotumia Viwango vya Kimataifa vya Ripoti za Kifedha (IFRS).

Akizungumzia vigezo vilivyotumika kupata washindi, Mkurugenzi Mtendaji wa NBAA, Pius Maneno, alisema walipatikana kwa kuangalia waliovuka asilimia 75 ya vigezo vilivyowekwa, ambako alipongeza kazi nzuri iliyofanywa na kampuni na taasisi zilizoshinda. Tuzo hizo hutolewa na NBAA kila mwaka kwa ajili ya kutambua na kuthamini ubora wa ripoti za kifedha kwa kampuni za umma, binafsi na taasisi ambazo zimekuwa zikikaguliwa na kutambuliwa kitaifa na kimataifa.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hizo, Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB, Benedicto Baragomwa, alisema wao kama wataalamu wa masuala ya fedha, wanatambua umuhimu wa kuandaa vitabu vya akaunti vya kampuni kwa njia na mifumo inayokubalika ngazi ya kimataifa.

"Ushindi huu unadhihirisha namna ambavyo tumejikita katika kudumisha uadilifu wa hali ya juu kwenye uwasilishaji wa taarifa zetu za kifedha za mwaka," alisema baada ya kupokea tuzo mbili kutoka kwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Amina Shabani.

# Jaka Mwambi afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Niabu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Kepteni Jaka Mwambi, amefariki dunia.

Kwa mujibu wa taarifa zilizothibitishwa na mtoto wake, Juvenile Mwambi, kiongozi huo aliyewahi kuwa Mkuu wa mikoa ya Tanga, Rukwa na Iringa alikutwa na mauti jana. Aidha, wakati wa uhai wake aliwahi kuwa Balozi wa Tanzania nchini Urusi, wakati wa serikali ya awamu ya nne.

Katibu Mkuu mstaafu wa CCM, Yusuph Makamba, alituma salamu za pole kwa familia, huku akimwelezea kiongozi huyo kuwa walifahamiana wakiwa chuo cha kijeshi Monduli, mkoani Arusha.

"Wakati wa vita tulikuwa wote makamisaa chini ya Brigedia Moses Nnauye, nilipokuwa Katibu Mkuu wa CCM, Mwambi alikuwa mchapakazi, mkereketwa wa hali ya juu na mbunifu sana," alisema Mzee Makamba.

# Ardhi yatoa matokeo utafiti kuboresha mapato

**Na Romana Mallya**

CHUO Kikuu cha Ardhi kimetoa matokeo ya utafiti uliofanywa kwenye maeneo sita yakiwamo ya kusaidia mamlaka za serikali kuboresha ukusanyaji mapato.

Alisema miongoni mwa utafiti uliofanywa na chuo hicho ni unaohusu vyanzo vya majanga kama mafuriko, lengo likiwa ni kubaini njia bora za kuwashirikisha wadau kutambua, kujilinda na kukabiliana na matatizo hayo. Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Evaristo Liwa, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya 13 ya chuo hicho.

Wanafunzi 977 walitunukiwa Shahada na Stashahada ikiwa 916 Shahada za awali, 45 Shahada za Uzamili na 10 Shahada za Uzamivu.

Idadi hiyo inajumuisha wahitimu sita wa Stashahada ya GFM4 ambao walitunukiwa Stashahada zao Julai 19, mwaka huu.

Pia alisema chuo kimefanya utafiti wa mfuko wa kubaini makazi yote katika Jiji la Dar es Salaam ambao ulihusisha picha za satelaiti.

"Chuo kilibaini kuwa mfumo huo wa kimakazi utasaidia taasisi za serikali kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasco), kuboresha hatua za ukusanyaji mapato," alisema.

Utafiti mwingine ni wa kuboresha matumizi ya maji ya umwagiliaji ya Bonde la Mto Rufiji, ili kuleta tija na kuongeza uzalishaji Wilaya ya Iringa na kutatua changamoto ndani ya bonde hilo.

"Utafiti wa ufumbuzi mahsusi wa mwenendo endelevu wa ukuaji wa miji katika Afrika ukihusisha utaratibu na uzoefu wa jamii husika katika upangaji miji.

"Lengo la utafiti huu ni kuwa daraja kati ya hali halisi ya ukuaji wa miji ya Afrika kwa sasa na mapendekezo ya utafiti ulizowahi kufanyika kuhusiana na ukuaji wa miji."

Prof. Liwa alitaja utafiti kuhusu ukuaji wa miji midogo ikiwamo kujifunza na kuzuia changamoto za ukuaji holela katika miji 20.

"Utafiti huu ulifanyika katika miji iliyo kwenye mchakato wa upangaji miji ikiwamo Mafinga, Ifakara, Geita na Gairo, lengo ni kubaini moduli bora ya kupanga na kuendeleza miji hii inayokuwa kwa kasi," alisema.

Pia alisema chuo hicho kimefanya utafiti kuhusu teknolojia ya kuhuisha matumizi ya mabaki ya kilimo ili kuleta tija kwa wahitimu na wakulima wadogo Mbarali, Mbeya.

"Utafiti huu uliofanyika katika miji midogo tisa ya Mbarali, utaleta mabadiliko chanya katika matumizi ya mabaki ya pumba za mchele ili kuzalisha mkaa wa kisasa," alisema.

Prof. Liwa alisema utafiti huo umezalisha mradi mkubwa wa kimkakati wa upimaji, upangaji ardhi na urasilimishaji wa makazi ili kupata hati za viwanja kwa wakazi.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**au piga simu: 0782253676**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**

**MAOMBI NA:169/2016**

JOHANES LEBELELA..............................MDAI

DHIDI YA

1. BRANDINA NKOFU
2. GODFREY MUTAKUBWA...............WADAIWA

KWA: BRANDINA NKOFU NA GODFREY MUTAKUBWA
(POPOTE PALE MLIPO)

Mnaarifiwa/unaarifiwa kuwa Maombi Na.169/2016 yamepangwa kutajwa tarehe 13.01.2020 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, R. MTEI saa 2.00 asubuhi

Hivyo,unaamuliwa/mnaamuliwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako/wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria/msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako/yenu na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 29/11/2019

---

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY
IN THE RESIDENT MAGISTRATES COURT OF TANZANIA
AT BUKOBA

RM CIVIL CASE NO.9/2019

IGOMA KOLPING SAVING AND
COOPERATIVE SOCIETY L.T.D CR EDIT...PLAINTIFF

VERSUS

JULIUS. M.APRONARY.....................DEFENDANT

TO, JULIUS. M.APRONARY

**RE: NOTICE OF DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned Appellant has lodged a case registered as Civil Case No. 9 of 2019 against you at the Resident Magistrates Court of Tanzania at Bukoba.

Take notice that the above said case has been scheduled for hearing on 12th day of DECEMBER, 2019 at 08:30 am before Hon. E. P. MPABANSI. You are authorized to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.

Given under my hand and seal of the court this 6th day of December,2019.

---

***Uza, Chenye Thamani Kubwa***

***Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

---

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# KLOPP: SALAH SASA YUPO FITI KINOMA



**LIVERPOOL,** England

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mohamed Salah hatimaye amerudi kuwa "fiti kwa asilimia 100", kwa mujibu wa kocha wake, Jurgen Klopp.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri alifunga bao la mwisho wakati Liverpool wakiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Bournemouth na kuweka rekodi ya kushinda michezo 15 kati ya 16 kwenye Ligi Kuu ya England.

Salah alifunga bao hilo la 63 katika mchezo wake wa 100 wa Ligi Kuu na kuuungana na wachezaji watatu Alan Shearer (79), Ruud van Nistelrooy (68) na Sergio Aguero (64) - ambao wamefunga mabao mengi katika mechi 100 za Ligi hiyo.

Salah alikuwa akisumbuliwa na maumivu ya kifundo cha mguu alichoumia kwenye mchezo dhidi ya Leicester City alipogongana na Hamza Choudhury Oktoba mwaka huu na Klopp sasa anajiamini kuwa mchezaji wake yupo fiti.

"Anaonekana kuwa fiti kwa asilimia 100," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni muda kidogo wakati alipoonekana kuumia, lakini kwa sasa naweza kusema yupo fiti kabisa tena kwa asilimia 100."

## Rodgers awapiku Klopp, Solskjaer

**LEICESTER,** England

BRENDAN Rodgers baada ya kusaini mkataba mpya na klabu ya Leicester City sasa anakuwa kocha namba tatu anayelipwa mshahara mkubwa zaidi kwenye Ligi Kuu England.

Kocha huyo alikuwa akihusishwa na kuhamia Arsenal baada ya timu hiyo kumfuta kazi aliyekuwa kocha wao Unai Emery. Lakini, sasa Rodgers ameamua kubaki zake pale kwenye dimba la King Power.

Mkataba huo mpya, sasa unamfanya Rodgers apandishe mshahara wake kutoka pauni milioni 5 kwa mwaka hadi pauni milioni 10.

Mshahara huo unamfanya Rodgers awe anazidiwa na Pep Guardiola na Jose Mourinho peke yao kwa makocha wanaolipwa fedha ndefu kwenye Ligi Kuu England.

Guardiola ndiye anayelipwa mshahara mkubwa zaidi, pauni milioni 20 kwa mwaka huko Manchester City.

Mourinho anashika namba mbili alikipwa pauni milioni 15 kwa mwaka pale Tottenham Hotspur licha ya kufukuzwa kazi kwenye klabu mbili zilizopita.

Kisha anafuata Rodgers na baada ya hapo wanafuata makocha wengine akiwamo Jurgen Klopp wa Liverpool, anayelipwa pauni milioni 7.5 kwa mwaka kama anavyolipwa Ole Gunnar Solskjaer pale Manchester United.

Baada ya hapo ni kocha wa West Ham United, Manuel Pellegrini, anayelipwa pauni milioni saba, kisha kocha wa Southampton, Ralph Hasenhuttl, anayepokea pauni milioni sita kwa mwaka na Frank Lampard akilipwa pauni milioni 5.5 milioni kwa mwaka pale Chelsea.





## Ni rasmi Aubameyang anaondoka

**LONDON,** Engaland

NI wazi kwamba sasa Pierre-Emerick Aubameyang anajipanga kuachana na Arsenal baada ya kujitoa kwenye mazungumzo ya kuhusu mkataba mpya kwenye kikosi hicho cha Emirates.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon, Aubameyang amefunga mabao 53 katika mechi 83 alizoitumikia Arsenal tangu alipojiunga nayo Januari 2018 akitokea Borussia Dortmund, lakini anataka kuondoka kwa sababu anahitaji timu inayoshindania mataji.

Na sasa mipango yake ni kuachana na wababe hao wa Emirates kwenye dirisha lijalo la majira ya kiangazi mwishoni mwa msimu huu.

Aubameyang alishinda Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu England msimu uliopita na msimu huu ameonyesha kuwa moto akiwa amefunga mabao 12 katika mechi 17 alizoitumikia timu hiyo ya London.

Mkataba wake umebakiza miezi 18 tu kufika tamati, lakini hali yake ya mambo huko kwenye kikosi hicho ipo njiapanda akitaka kuondoka zake kutokana na mambo kutoeleweka. Aubameyang alinaswa kwa pauni milioni 56, lakini anaona kila siku timu inazidi kurudi nyuma tu na yeye mipango yake ni kubeba mataji.

Kwenye maisha yake ya soka, Aubameyang, amebeba Kombe la Ligi Ufaransa na Kombe la Ujerumani, hivyo anataka kunyakua taji kubwa zaidi kabla ya kuachana na mchezo huo, ambapo ikifika Juni mwakani atafikisha umri wa miaka 31.

Aubameyang anaripotiwa kutaka kuondoka wakati zimepita wiki chache tu tangu alipoteuliwa kuwa nahodha kwenye kikosi hicho. Arsenal imeshinda mechi nne tu kati ya 15 ilizocheza kwenye Ligi Kuu England na kesho Jumatatu watakuwa na shughuli ya kuwakabili West Ham United ugenini.

# JOSHUA AMTWANGA RUIZ JR




**AD DIRIYAH,** Saudi Arabia

BONDIA wa ngumi za kulipwa za uzito wa juu, Anthony Joshua amefanikiwa kumtwanga mpinzani wake wa karibu Andy Ruiz Jr kwa pointi kwenye pambano lililopigwa katika Uwanja wa Ad Diriyah, mjini Saudi Arabia usiku wa kuamkia jana.

Pambano hilo la uzito wa juu lilikuwa la marudiano na mabondia hao walikuwa wanawania mikanda ya WBA, WBO na IBF iliyokuwa mikononi mwa Ruiz Jr ambaye aliitwaa baada ya kumtwanga Joshua raundi ya saba kwenye pambano la awali lililopigwa Juni, Mosi mwaka huu.

Ushindi huo unamfanya Joshua ambaye ni namba tatu kwa ubora duniani kwa ngumi za uzito wa juu, kurudisha mikanda yake yote mitatu aliyoipoteza wakati alipochapwa kwenye pambano la awali na Ruiz Jr maarufu kama kibonge mwepesi.

Pambano hilo lililokuwa la raundi 12, Joshua alipata jumla ya pointi 118, huku Ruiz Jr akijipatia jumla ya pointi 110.

Baada ya Joshua ambaye ni raia wa Uingereza mwenye asili ya Nigeria kupoteza pambano lake la kwanza katika kwa kupigwa na bondia kutokea Marekani mwenye asili ya Mexico Andy Ruiz, alikubali kurudiana naye ili kujiuliza alikosea wapi.

Promota maarufu anayemsimamia Joshua kuandaa mapambano mbalimbali, Eddie Hearn alitangaza kuwa atarudiana tena na Ruiz katika kipindi cha Novemba au Desemba kwani kipengele cha mkataba wao kinawaruhusu kurudiana kama mmoja wao atahitaji.

Pambano la juzi lilikuwa na msisimko wa aina yake kutokana na mabondia wote kupaniana na kupamba vyombo vya habari.

Awali Ruiz alionekana kumshambulia kwa kasi katika raundi za kwanza, lakini hakuwa na uwezo wa kumpiga na Joshua alikuwa mvumilivu na kuweza kujibu mashambulizi kwenye raundi za mwisho na hatimaye kuibuka mshindi.

# Benzema aibeba Real

**MADRID,** Hispania

KARIM Benzema alifunga na kutoa pasi ya mwisho 'assist' wakati Real Madrid wakiibuka na ushindi dhidi ya Espanyol, lakini walimaliza wakiwa wachezaji 10 uwanjani baada ya Ferland Mendy kutolewa nje.

Kwa sasa anashika nafasi ya pili kwa kufunga mabao mengi kwa Ligi Kuu ya Hispania, akicheka na nyavu mara 11, akipitwa na nyota wa Barcelona, Lionel Messi mwenye mabao 12.

Benzema alimtengeneza bao mchezaji mwenzake, Raphael Varane aliyefunga la kwanza na yeye akafunga la pili na kufanya matokeo kuwa 2-0 zikiwa zimesalia dakika 10 mpira kumalizika.

Mshambuliaji huyo pia alipoteza nafasi katika kipindi cha pili kwa kupiga mpira uliomlenga golikipa, Diego Lopez.

Mendy alionyeshwa kadi ya pili ya njano katika dakika ya 82 kwa kucheza faulo na hivyo kupata kadi nyekundu.

Ushindi huo uliwapeleka Real Madrid kileleni mwa msimamo kwa muda kabla ya Barcelona kurudi tena baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 5-2 dhidi ya Mallorca.

Benzema ambaye ni raia wa Ufaransa msimu huu unaonekana kuwa mzuri zaidi kwake akiwa ndiye mfungaji wa mabao ya Real Madrid karibia katika kila mechi.





# *Guardiola: Haikuwezekana kuwazuia Man United*

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema kuwa Manchester City wasingeweza kuzuia presha ya mashambulizi ya wachezaji wa Manchester United kwenye mchezo wao wa 'dabi' juzi Jumamosi wakati wakiambulia kipigo cha 2-1.

Wageni United walionekana kulisakama lango la wapinzani wao kwa dakika nyingi katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Etihad, na kuwasaidia kupata mabao mawili katika kipindi cha kwanza.

Marcus Rashford alishinda na kufunga penalti kabla ya Anthony Martial kufunga la pili akipokea pasi ya Daniel James.

Guardiola alizungumzia safu ya ushambuliaji ya United na kusema kwamba wasingeweza kuwazuia kwa sababu mashambulizi yalikuwa makali kwao.

"Nilipenda jinsi timu yangu ilivyocheza," alisema akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo. "Tulishindwa kuzuia kasi ya mashambulizi yao, kwa uhakika walikuwa juu yetu kwa mchezo tofauti na tulivyocheza nao mwaka jana.

"Tulijua kwamba, kasi yao ilikuwa kubwa, wakiwa na James, Martial na Rashford, lakini kiukweli kabisa tulishindwa kuwazuia na lilikuwa jambo lisilowezekana."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI AVUNJA REKODI YA HAT-TRICK ZA RONALDO

## Ni ya 35 kwenye La Liga, pia awa mchezaji wa kwanza kwenye ligi tano bora Ulaya aliyefunga...

**BARCELONA,** Hispania

LIOEL Messi ameipiku rekodi ya Cristiano Ronaldo kwa kufunga 'hat-trick' nyingi zaidi kwenye historia ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, baada ya kufunga mabao matatu wakati Barcelona ikishinda 5-2 dhidi ya Real Mallorca juzi, Jumamosi.

**Katika wiki ambayo pia ametoka kumzidi mpinzani wake Ronaldo kwa kutwaa tuzo ya Ballon d'Or ya sita, Messi alionyesha kwa nini alichaguliwa kuwa mchezaji bora wa dunia kwa kuonyesha kiwango cha ku vutia katika mchezo huo uliopigwa dimba la Camp Nou.**

Mchezaji huo mwenye umri wa miaka 32, alifunga mabao mawili kwa mashuti ya mbali katika kipindi cha kwanza na aliongeza la tatu dakika saba kabla ya mchezo kumalizika na kufikisha 'hat-trick' ya 35 kwenye Ligi Kuu ya Hispania.

Hiyo ina maana sasa amemzidi Ronaldo kwa hat-trick moja ambaye alitumia miaka tisa pale katika klabu ya Real Madrid kabla ya kujiunga na miamba wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus mwaka 2018.

Bao la kwanza la Messi lilimfanya pia kuwa mchezaji pekee kufunga zaidi ya mabao 10 kwa kila msimu 14 iliyopita kwenye ligi tano kubwa za Ulaya.

Ushindi huo uliwarudisha Barca kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu wakiwazidi Real Madrid kwa tofauti tu ya mabao ya kufunga na kufungwa, huku wakielekea kwenye mchezo wa kwanza wa Clasico msimu huu baadaye mwezi huu.

Kocha wa Barcelona, Ernesto Valverde alisema rekodi ya Messi ya kufunga 'hat-trick' nyingi ilikuwa "nzuri kusherehekea tuzo ya Ballon d'Or".

Baada ya kushinda tuzo yake ya sita ya Ballon d'Or mapema wiki jana, Messi akajifungia mabao matatu kwa mabingwa hao wa La Liga, Barca na kuwa ushindi huo wa 5-2.

Ushindi huo wa Messi wa Ballon d'Or ulimfanya kumpiku mpinzani wake Ronaldo, na nahodha huyo wa Barca akavunja rekodi ya mchezaji wa zamani wa Real Madrid.

Baada ya kuvunjwa kwa reodi hiyo, Valverde alimsifia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Siamini," alisema Valverde akiwaambia waandishi wa habari baada ya Barca kurudi kileleni mwa msimamo."Ilikuwa njia nzuri ya kusherehekea tuzo ya Ballon d'Or."

Huku Messi akitawala vyombo vya habari kwa tuzo hiyo, mchezaji mwenzake wa Barca, Luis Suarez alifunga bao kwa kisigino.

Suarez alifunga bao hilo dakika ya 43 na Valverde alisema: "Goli lile lilinishangaza, sababu mimi nilijua ni pasi kwa mchezaji mwenzake."

## ZISIKUPITE

### BALE AGEUZWA CHAMBO REAL

REAL Madrid inaandaa kumtoa ofa mshambuliaji Mcolombia James Rodriguez, 28, na winga wa Wales, Gareth Bale, 30, kama sehemu ya mpango wa kubadilishana na kiungo wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba, 26. ***(Eldesmarque, via Express)***

### VIDAL AWEKWA SOKONI BARCA

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde amefunguka kuwa kiungo Arturo Vidal anaweza kujiunga na Manchester United, na pauni milioni 13 zipo mezani kwa nyota huyo wa Chile mwenye umri wa miaka 32. ***(Mirror)***

### YAMKOMALIA SANCHO

MKURUGENZI wa Michezo wa Borussia Dortmund, Michael Zorc, amesema mshambuliaji wa England, Jadon Sancho hataondoka klabuni hapo Januari, licha ya Manchester United kuhusishwa zaidi na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19. ***(Manchester Evening News)***

### KOVAC AIKANA EVERTON

KOCHA wa zamani wa Bayern Munich, Niko Kovac amekanusha kuwa yupo kwenye mbio za kwenda kuinoa Everton, licha ya hivi karibuni kuonekana jukwaani katika Uwanja wa Goodison Park akitazama wakati 'Toffees' hao wakishinda Jumamosi. ***(Goal)***

### SPURS YAMFUATA DEMIRAL

KOCHA Jose Mourinho kuhakikisha beki wa Juventus na Uturuki, Merih Demiral, 21, unakuwa usajili wake wa kwanza hapo Tottenham, na hivyo sasa klabu hiyo kujiunga katika mbio moja na Arsenal pamoja na Manchester United kwenye mbio za kumwania. ***(Sun)***

### POCHETTINO AIITA ARSENAL

KOCHA wa zamani wa Spurs, Mauricio Pochettino hawezi kuweka kando nafasi ya kwenda kuinoa Arsenal. ***(TYC Sports, via Mail)***

### BARCA KUMFUNZA ZAIDI MESSI

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu amesema anataka mshambuliaji Muargentina Lionel Messi, 32, kutia saini mkataba mpya. ***(Marca)***

### CHELSEA KUJITOSA KWA AKE

CHELSEA ipo tayari kutoa ofa ya pauni milioni 40 kwa mchezaji wa Bournemouth, Nathan Ake, 24, na klabu hiyo ya Stamford Bridge ikiwa tayari kutoa dau linalohitajika kuvunja mkataba wake. ***(Telegraph)***

### EVANILSON AIPAGAWISHA LIVER

LIVERPOOL inavutiwa na straika wa Fluminese, Evanilson, 20, ambaye atapatikana kwa uhamisho huru hapo Februari mwakani. ***(Netflu, via Sun)***

### NEWCASTLE YASAKA STRAIKA

NEWCASTLE inajiandaa angalau kusajili mshambuliaji mmoja katika dirisha la Januari, na straika wa Hull City, Jarrod Bowen, 22, akiwa katika rada za kocha Steve Bruce. ***(Telegraph)***

### ASTON VILLA, CELTIC VITANI

BEKI wa kulia wa Olympiacos, Omar Elabdellaoui anawindwa na Aston Villa na Celtic na nyota huyo wa kimataifa wa Norway amesema ana "malengo" ya kutua. ***(Birmingham Live)***

HABARI MICHEZO

## Wadau waichangia Z'bar Heroes ikiivaa Kili Stars leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI jana timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes) ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Sudan kwenye mechi ya kuwania Kombe la Chalenji nchini Uganda, wadau mbalimbali wa soka visiwani hapa wameendelea kujitokeza kuichangia ili ifanye vizuri kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa).

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Seif Kombo Pandu, alisema wadau mbalimbali wamehamasika katika kuichangia timu hiyo ili iweze kufanya vizuri katika michuano hiyo inayoendelea nchini Uganda, ambapo kesho itashuka dimbani kuwavaa ndugu zao wa Tanzania Bara, Kilimanjaro Stars.

Alisema hamasa iliyopatikana kwa mwaka huu imewatia moyo wachezaji na hata viongozi wa ZFF hususan katika kuhakikisha timu za taifa zinafanya vizuri na maandalizi ya mapema katika michuano ambayo inawakilisha nchi.

Alisema michango hiyo ambayo ilitolewa na taasisi za serikali, watu binafsi na wafanyabiashara itahudumia timu baadhi ya mambo ambayo yanatakiwa wajihudumie wenyewe wakati wakiwa katika mashindano.

Aidha, alisema jamii ya wapenda soka wamehamasika kununua jezi za timu ya Taifa ya Zanzibar iliyozinduliwa katika Uwanja wa Amaan hali hiyo imeleta faraja kuwa soka ndio kitu kikubwa kinachopendwa visiwani Zanzibar.

## Mtango ulingoni na Mthailand Mkwakwani

**Na Boniface Gideon,** TANGA

MKOA wa Tanga unatarajiwa kusimama kwa muda kushuhudia pambano la ngumi kati ya bondia namba 50 duniani, Mthailand Amnat Ruenroeng, ambaye alishikilia ubingwa wa IBF kuanzia mwaka 2014 hadi 2016 wakati atakapozichapa na bondia machachari nchini, Salim Mtango Januari 31, mwakani.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, mwandaaji wa pambano hilo, Ally Mwazoa, alisema baada ya kuona Mkoa wa Tanga unavipaji vingi vya mabondia, ameamua kujitolea kuwatangaza kimataifa ili waweze kupanda viwango kimataifa na kwamba pambano hilo litapigwa katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

"Nimeona mkoa wetu unavipaji vingi vya ngumi, hivyo nimeamua kuwatafutia mapambano ya kimataifa, bondia huyu anashika nafasi ya pili huko Thailand na anashika nafasi 50 duniani katika ubingwa wa 'UBO' na tunaamini bondia wetu akishinda atapanda viwango," alisema Mwazoa.

# TANZANIA U-17 WANAWAKE KUIVAA ERITREA CHALENJI

**Na Mwandishi Wetu,** JINJA

TIMU ya soka ya wasichana wa umri chini ya miaka 17 ya Tanzania Bara, inatarajia kuanza kampeni ya kuwania ubingwa wa mashindano ya Kombe la Chalenji kwa vijana kwa kupambana dhidi ya wenzao wa Eritrea katika mchezo wa kwanza utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Njeru mjini hapa.

**Mechi hiyo ya yosso wa Tanzania Bara itaanza kuchezwa kuanzia saa 5:00 asubuhi na kufuatiwa na mchezo kati ya Djibouti dhidi ya Kenya (saa 7:30 mchana) na wenyeji Uganda watakaowakaribisha Burundi kuanzia saa 10:00 jioni.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu ya Tanzania Bara, Bakari Shime, alisema wamejiandaa vema na mashindano hayo baada ya kufanya mazoezi kwa muda wa wiki saba.

Shime alisema anaamini wachezaji wake watatafsiri vizuri mafunzo waliyopata na kubwa kurekebisha makosa ambayo "dada zao" Kilimanjaro Queens waliyafanya katika fainali za Kombe la Chalenji za Wanawake zilizopita.

Alisema hana majeruhi katika kikosi chake na anatarajia kukutana na ushindani katika mechi zote watakazocheza, kutokana na wapinzani wao kujipanga kupambana na Tanzania.

"Tumejiandaa vizuri na mashindano haya, naweza kusema ndio timu iliyofanya mazoezi kwa muda mrefu, lakini najua tutaingia tukiwa na presha ya kusaka matokeo mazuri, huku tukifahamu timu zote zitaingia zikipambana kutufunga, ni wazi katika ukanda huu, Tanzania tumekuwa na rekodi nzuri katika soka la wanawake," alisema Shime.

Nahodha wa timu hiyo, Irene Kisisa, alisema wachezaji wote wako tayari na wanachofikiria ni kupambana ili kutwaa ubingwa wa michuano hiyo.

"Tunashukuru kupata nafasi hii, tumefanya mazoezi na tumepata maandalizi mazuri, tunachowaahidi Watanzania ni kurudi na ubingwa," alisema Kisisa.

Mashindano hayo yanayofanyika kwa mara ya kwanza kwenye ukanda huu, yataendelea tena keshokutwa kwa Tanzania Bara kucheza dhidi ya Burundi wakati Kenya watawakaribisha Eritrea na Uganda watavaana na Djibouti.



MC Mziwanda, ambaye atapamba sherehe za Uhuru jijini Mwanza leo na wimbo wake wa 'Magufuli Kimbunga', akiwa katika moja ya matamasha yake hivi karibuni. **PICHA: MAKTABA**

# *Mziwanda kuimba 'Magufuli Kimbunga'*

**Na Sabato Kasika**

MSHEREHESHAJI maarufu jijini Mwanza, Emmalactony Mziwanda maarufu MC Mziwanda, ambaye ni muimbaji, amepata shavu la kuimba wimbo wake wa "Magufuli Kimbunga", mbele ya Rais John Magufuli kwenye kilele cha sherehe za miaka 58 ya Uhuru wa Tanzania.

Sherehe za miaka 58 ya Uhuru zitafanyika kitaifa jijini Mwanza leo, huku MC Mziwanda akiwa miongoni mwa wale watakaotoa burudani kwa wimbo wake huo mpya utakaosikika kwa mara ya kwanza.

"Mimi ni mshereheshaji na mwimbaji wa nyimbo za Injili, lakini nimetunga wimbo huo wa "Magufuli Kimbunga" na kupewa nafasi ya kutumbuiza katika sherehe hizo za Uhuru," alisema MC Mziwanda.

Amesema alipeleka wimbo huo kwenye kamati ya maandalizi ya sherehe ikausikiliza na kuupitisha kwa vile una ujumbe na maudhui yaliyomo yakibainisha shughuli zilizofanywa na serikali ya awamu ya tano.

"Wimbo umetanabaisha shughuli zote zilizofanywa na Rais John Magufuli na ni wenye hamasa kubwa, ndiyo maana nikapata nafasi hiyo ambayo ni adimu, hivyo ninaona fahari kuipata kwa mara ya kwanza," alisema.

Amesema anaona fahari wimbo wake kukubalika na inampa hamasa ya kuendelea kuandaa nyingine zaidi zenye maudhui, na kwamba kwake ni fahari kuimbe mbele ya Rais.

Mbali na wimbo huo, MC Mziwanda amekamilisha pia nyimbo za Injili alizozipa majina ya 'Mungu Yuko Hapa', 'Sema Nasi', 'Shuka Baba na 'Ulinzi' ambao utakuwa umebeba jina la albamu.

# Michezo

Jumatatu Desemba 9, 2019

Nipashe




Messi avunja rekodi ya hat-trick za Ronaldo HABARI UK.30

LA SHAVUNI...



Bondia Anthony Joshua (kulia) akimpelekea konde la shavuni mpinzani wake, Andy Ruiz Jr katika pambano la uzito wa juu kuwania mikanda ya WBA, WBO na IBF lililofanyika katika Uwanja wa Ad Diriyah, mjini Saudi Arabia usiku wa kuamkia jana. Joshua alishinda kwa pointi. **HARABARI UK. 29**

## Kili Stars yapigwa, Zanzibar angalau

**Na Somoe Ng'itu,** KAMPALA

TIMU ya Soka ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), imeanza vibaya kampeni ya kuwabia ubingwa wa mashindano ya Kombe la Chalenji baada ya kukubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Kenya (Harambee Stars).

Mabingwa hao watetezi, wamepata ushindi huo kupitia kwa Hassan Abdallah, aliyefunga bao pekee katika mchezo huo dakika ya nne baada ya kuwatoka mabeki wa Kilimanjaro Stars na kuachia shuti kali lililojaa moja kwa moja wavuni.

Kwa matokeo hayo, Harambee Stars inaongoza Kundi B la michuano hiyo iliyoandaliwa na Baraza la Vyama vya Michezo Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), kufuatia ushindi huo walioupata katika Uwanja wa Lugogo jijini Kampala, Uganda.

Nafasi ya pili inashikwa na Sudan na Zanzibar Heroes ambazo katika mechi ya mapema mchana jana, zilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Sudan na hivyo kugawana pointi.

Stars itashuka tena dimbani kesho kuivaa Zanzibar kabla ya kucheza na Sudan kwenye mchezo wa mwisho wa hatua ya makundi.

Katika mchezo huo, timu zote zilianza kwa kasi na dakika ya pili Kilimanjaro Stars ilikaribia kupata bao kupitia kwa Miraji Athuman, lakini mpira aliopiga kutoka wingi ya kulia ulikuwa mwingi na kutoka nje.

Dakika ya 14 Abdallah alipata nafasi ya kufunga, lakini safari hii akiwa jirani na kipa Aishi Manula shuti lake likapaa juu na kutoka.

# MO ACHARUKA ATANGAZA WACHEZAJI WAKUTIMULIWA

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

## ●●● Mzimu wa UD Songo bado wamtesa, kocha mkuu sasa kutangazwa Jumatano akianza na Yanga...

MWEKEZAJI wa Simba na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo, Mohamed "Mo" Dewji, ametoa ya moyoni kwa kueleza kutoridhishwa na nidhamu mbovu inayoonyeshwa na baadhi ya wachezaji wa klabu hiyo kwa siku za hivi karibuni, huku akitangaza sasa timuatimua itawakumba wale wote wenye utovu wa nidhamu ikiwa ni baada ya kumkumba Kocha Mkuu, Patrick Aussems.

**Kumekuwa na minong'ono kuwa baadhi ya wachezaji wa Simba wamekuwa na utovu mkubwa wa nidhamu hasa nje ya uwanja kiasi cha kusababisha viwango vyao ndani ya uwanja kushuka kwa kiwango kikubwa.**

Akizungumza kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa klabu hiyo kongwe nchini, Mo alisema uwekezaji mkubwa na uwezo wa kifedha walionao kwa sasa, Simba umegeuka kama fimbo ya kuwachapia.

"Siridhishwi hata tone na nidhamu ya baadhi ya wachezaji wetu nje ya uwanja. Nimekuwa mnyonge kuona uwekezaji tuliouweka kwao, baadhi yao, huutumia kama fimbo ya kutuchapia," alisema na kuongeza.

"Niwaambie wachezaji wote, Simba ni klabu kubwa kweli kweli, tena kubwa hasa, na hakuna shaka ni namba moja Afrika Mashariki, bodi ninayoiongoza mimi haitavumilia mchezaji yeyote asiyejua thamani ya Simba. Kuonyana sasa imetosha," alisisitiza.

Mwenyekiti huyo alisema kama klabu inawalipa vizuri, wachezaji nao wana wajibu wa kulipa matokeo ya furaha na si vinginevyo.

"Sisi tunawalipa vizuri mno, na wao wana wajibu wa kutulipa matokeo na furaha. Na ili furaha iwapo, lazima nidhamu isimamiwe kikamilifu, na katika hili hatutanii. Hatutajali ukubwa wa jina la mchezaji yeyote," alisema mbele ya wachezaji wa klabu hiyo ambao walikuwapo kwenye mkutano huo, ukiondoa wale walio kwenye timu ya Tanzania Bara, Kilimanjaro Stars inayoshiriki michuano ya Chalenji nchini Uganda.

"Nidhamu kwetu ni muhimu kama tunataka tufikie malengo tuliyokusudia. Na haya ndio yaliyotufanya bodi tuchukue maamuzi magumu kwa kocha wetu. Timu imeshindwa kufikia malengo, kisa nidhamu hakuna, halafu tuvumilie?"

Alisema binafsi hajakaa sawa tangu timu hiyo itolewe na UD Songo kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Binafsi bado sijakaa sawa hadi leo baada ya matokeo ya mechi yetu dhidi ya timu ya UD Songo. Nilikuwa sipo nchini. Baada ya mechi ile kuisha, nililia mno."

Na kuelekea mechi ya watani wa jadi Januari mwakani, Ofisa Mtendaji wa Simba, Senzo Mazingisa amesema maandalizi ya mechi hiyo dhidi ya Yanga yamekamilika na taarifa rasmi ataitoa Jumatano ikiwa ni pamoja na kumtangaza kocha mkuu atakayeiongoza miamba hiyo.

"Simba ni timu kubwa katika soka la Afrika. Ni jukumu letu sote, hasa kwa wachezaji kufanya vizuri ndani ya uwanja na kuifanya iendelee kutambulika kama klabu kubwa."

"Tuna mchezo muhimu dhidi ya watani wa jadi Januari. Napenda kuwahakikishia kuwa maandalizi na mambo yote ya mchezo huo yapo tayari. Wachezaji watakuwa kambini na tangazo la nani atakuwa kocha mkuu mpya na benchi la ufundi litatoka rasmi Jumatano ijayo."

Kwa upande wake Kaimu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Mwina Kaduguda amesema katika uongozi wake atajikita zaidi kwenye uchumi wa timu hiyo, lengo likiwa ni kuifanya iwe juu zaidi.

"Tunataka kuwa na matawi ambayo yatauza bidhaa za Simba vile vile itasaidia vijana kupata ajira kupitia matawi hayo," alisema Kaduguda.

Alisema ataboresha maisha ya wanachama pamoja na mashabiki wao na kuwataka wamtunze mwekezaji wao Mo Dewji kama dhahabu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >